**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

______________________

# TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KUHUSU UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU NA BAJETI YA OFISI YA WAZIRI MKUU – TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA FEDHA 2025/2026 PAMOJA NA MAONI YA KAMATI KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

______________________

*(Kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la 2025)*

Ofisi ya Bunge,
10, Barabara ya Morogoro
S.L.P. 941
40490 Tambukareli
**DODOMA**

**APRILI, 2026**

# YALIYOMO

**YALIYOMO** ........ **i**
**SEHEMU YA KWANZA** ........ **1**
1.0 **UTANGULIZI** ........ **1**
**SEHEMU YA PILI** ........ **2**
2.0 **MAELEZO NA UCHAMBUZI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** ........ **2**
2.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha na kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ........ 2
2.1.1 Ujenzi wa Stendi ya Mabasi – Mikumi ........ 3
2.1.2 Utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Barabara za Mikumi Mjini *(Upgrading of Mikumi Town Roads 1.45 km to Rigid Pavement in Kilosa District)* (Mradi Na. S01/014/2024/2025/W/73) ........ 7
2.1.3 Kuendeleza Ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Morogoro (Mradi Na. 3249) ........ 9
2.1.4 Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji kwa ushindani Manispaa ya Morogoro (Mradi LGA/079/2022/2023/HQ/W/16/PCKG/01) ........ 12
2.1.5 Ujenzi wa Barabara ya Picha ya Ndege – Bokotimiza (0.52km) kwa kiwango cha lami ........ 14
2.1.6 Ujenzi wa Barabara ya Kongowe – Forest – Yombo (0.7km) kwa kiwango cha Lami. ........ 16
2.1.7 Ujenzi wa Barabara ya Bomang'ombe – Kikavuchini kwa kiwango cha Lami (3.5km) (Mradi Na. S10/009/2023/2024/W/229) ........ 18
2.1.8 Ujenzi wa Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia (Mradi Na. 4390) ........ 19
2.1.9 Ujenzi wa Shule Mpya ya Msingi ya Mkondo Mmoja - Shule ya Msingi Lowasa (Mradi Na. 4312) ........ 23
2.1.10 Ujenzi wa Sekondari ya Migungani (Mradi Na. 4390) ........ 25
2.1.11 Ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi yaendayo Mikoani (*Bondeni City Bus Terminal*) (Mradi Na. 7003/TACTIC/P171189/2024-2025/W/01) ........ 26
2.1.12 Ujenzi wa Soko la kwa Mrombo ........ 28
2.1.13 Ujenzi wa Soko la Kilombero ........ 30
2.1.14 Mradi wa Uboreshaji wa Bustani ya Mapumziko Themi (*Themi living Garden*) ........ 33
2.2 Tathmini ya Jumla ya Utekelezaji wa miradi, kwa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kutembelewa na kukaguliwa na Kamati 34
2.2.1 Udhaifu wa Utekelezaji wa Miradi katika Mkoa wa Morogoro ........ 34
**SEHEMU YA TATU** ........ **36**
3.0 **UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026** ........ **36**
3.1 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka 2025/2026 ........ 36
3.2 Uchambuzi wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ........ 37
**SEHEMU NNE** ........ **51**

**4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027**........**51**
4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027........**51**
4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 – OWM-TAMISEMI........**56**
**SEHEMU YA TANO**........**61**
5.0 **MAONI NA USHAURI WA KAMATI**........**61**
**SEHEMU YA SITA**........**67**
6.0 **HITIMISHO**........**67**

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| **TAMISEMI** | : Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **OWM-TAMISEMI** | : Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa |
| **OPD** | : Out Patient Department |
| **BoQ** | : Bill of Quantities |
| **TARURA** | : Tanzania Rural and Urban Roads Agency |
| **TACTIC** | : Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness |
| **VETA** | Vocational Education and Training Authority |
| **SGR** | Standard Gauge Railway |
| **TFS** | Tanzania Forest Services Agency |
| **TPC** | Tanganyika Planting Company |
| **ATC** | Arusha Technical College |
| **TANROADS** | Tanzania National Roads Agency |
| **PCB** | Physics, Chemistry, Biology |
| **PCM** | Physics, Chemistry, Advanced Mathematics |
| **CBN** | Chemistry, Biology, Nutrition/Food Science |
| **DART** | Dar es Salaam Rapid Transit |
| **OC** | Other Charges |
| **TSC** | Teachers Service Commission |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **MC** | Municipal Council |
| **TC** | Town Council |
| **M&E** | Monitoring and Evaluation |

# SEHEMU YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 121(9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 ninatoa shukrani kwako kwa kunipa wasaa ili niwasilishe mbele ya Bunge lako Tukufu Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 pamoja na Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027.

**Mheshimiwa Spika**, Maeneo muhimu yanayoguswa na kuelezwa kwa kina na taarifa hii ni kama ifuatavyo: -

(a) Maelezo na uchambuzi kuhusu ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(b) Uchambuzi wa Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti na uzingatiaji wa Maoni ya Kamati kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;

(c) Uchambuzi wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 (Makadirio ya Maduhuli na Matumizi); na

(d) Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati.

## SEHEMU YA PILI

## 2.0 MAELEZO NA UCHAMBUZI KUHUSU UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 Ofisi ya Waziri Mkuu, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, iliidhinishiwa na Bunge jumla ya **shilingi 1,791,592,207,143.72** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuzingatia Kanuni ya 120 (1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025 Kamati ilitembelea na kukagua baadhi ya miradi hiyo ya maendeleo iliyotekelezwa na ofisi hii katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Miradi iliyotembelewa ni miradi ya elimu, afya, stendi za mabasi, masoko, pamoja na barabara zinazosimamiwa na Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini *(TARURA)*.

### 2.1 Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha na kutekelezwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa ilifanya ukaguzi wa baadhi ya miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika Mwaka wa Fedha 2025/2026. Ziara ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ilifanywa kwa kuzingatia Kanuni ya 120(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, 2025.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata wasaa wa kutembelea na kukagua miradi katika Mikoa minne ya Morogoro, Pwani, Kilimanjaro, na Arusha, ambako jumla ya miradi kumi na mbili (12) iliyotengewa fedha kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 ilikaguliwa. Matokeo ya uchambuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo: -

### 2.1.1 Ujenzi wa Stendi ya Mabasi – Mikumi

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa ujenzi wa Mradi wa Stendi ya Mabasi Mikumi unatekelezwa na Halmashauri ya Mji Mdogo wa Mikumi katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa.

**Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** mradi huu utakapokamilika utakuwa na manufaa yafuatayo: -

(i) Kuboresha huduma za usafiri kwa abiria kwa kuwapatia eneo salama na lenye miundumbinu bora ya kusafiria;

(ii) Kuongeza mapato ya Halmashauri kupitia ushuru, ada na kodi mbalimbali zitakazotokana na shughuli za usafiri na biashara ndani ya stendi;

(iii) Kutoa ajira zipatazo 195 za muda mfupi na ajira za muda mrefu zaidi ya 50 baada ya kukamilika kwa mradi.

(iv) Utaongeza usalama wa abiria na mali zao pamoja na kuchochea maendeleo ya kiuchumi katika kata ya Mikumi na maeneo ya Jirani.

**Hali ya Utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia wakati wa ukaguzi wa Kamati, mradi huu ulikuwa bado haujaanza kutekelezwa kutokana na fedha kutokupokelewa kutoka Hazina.

**Uchambuzi wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyo ada ya taratibu za ukaguzi wa miradi, baada ya kupokea taarifa hii ya mradi Kamati ilifanya

uchambuzi kuhusu na utekelezaji wa mradi huu. Katika uchambuzi wake Kamati imebaini masuala mbalimbali ya msingi kama ifuatavyo: -

**a) Umbali wa eneo inakotarajiwa kujengwa Stendi kutoka Barabara Kuu ya Morogoro – Iringa**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa Mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Mikumi umepangwa kujengwa katika eneo lililo mbali kwa mita 350 kutoka Barabara Kuu ya Morogoro – Iringa. Kwa hulka ya ujenzi wa stendi, eneo hilo ni mbali kutoka ilipo Barabara hiyo kuu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaka kujua sababu ya stendi hiyo kupelekwa umbali huo na kujibiwa kuwa ni kutokana na kukosekana kwa eneo lililo karibu na Barabara. Hata hivyo, Kamati ilibaini kuwa Halmashauri ina eneo lililo karibu na Barabara ambalo linatumika kama soko. Aidha, Kamati ilibaini kuwa eneo hilo linalotumika kama soko awali lilitengwa kwa ajili matumizi ya stendi. Kamati ilihoji sababu ya eneo hilo lililotengwa kwa ajili ya stendi kutumika kama soko na kujibiwa kuwa ni kutokana na wananchi wenyewe kuanza kutumia eneo hilo kwa shughuli za biashara.

**Mheshimiwa Spika,** vilevile, katika uchunguzi wake Kamati ilibaini kuwa wananchi walipewa eneo hilo ili litumiwe na wafanyabiashara ndogondogo kwa kujenga miundombinu isiyo ya kudumu. Kamati pia ilibaini kuwa, eneo linalotakiwa kujengwa Stendi ya Mabasi lilitengwa kwa ajili ya kuwa Bustani kwa wananchi kupumzika.

**b) Eneo la stendi kuwa Katikati ya makazi ya watu**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake Kamati ilibaini kuwa eneo inapotakiwa kujengwa stendi ni katikati ya makazi ya watu.

Hii inaweza kusababisha hatari pale mabasi yatakapoanza kuingia stendi huku maeneo hayo yakiwa na watu hasa watoto.

**Mheshimiwa Spika,** ni Dhahiri kuwa mabasi yatakayokuwa yanaingia katika stendi hiyo yatazalisha kelele. Hali hii si inaweza kusababisha matatizo ya afya ya mwili kwa wakazi wanaoishi maeneo ilipo stendi. Aidha, inaweza kuwasababishia ama kuwaongeza tatizo la afya ya akili.

**Mheshimiwa Spika,** kwa kuwa maeneo haya yana makazi ya watu, kupitisha mabasi na vyombo vingine vya usafiri katika maeneo hayo kunaweza kusababisha foleni na hivyo kuleta usumbufu kwa wananchi wakazi wa maeneo hayo. Aidha, ni dhahiri kuwa mabasi yatakayokuwa yanapita katika barabara za mitaa hiyo yanaweza kusababisha mtikisiko wa ardhi na hivyo kuweza kusababisha nyufa na hata hatari ya kubomoka kwa nyumba za wananchi.

**c) Udogo wa eneo inapotaka kujengwa stendi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa Mji Mdogo wa Mikumi unakua kwa kasi, hasa kutokana na kukua na kuongezeka kwa mizigo inayohudumiwa na Bandari ya Dar es Salaam, kuongezeka kwa shughuli za utalii na kukua kwa uchumi wa wananchi wa mji huo. Katika uchunguzi wake Kamati imebaini kuwa eneo inapotaka kujengwa stendi ni dogo. Kutokana na kwamba matarajio ya kukua kwa Mji Mdogo wa Mikumi ni makubwa. Kamati inaona kwamba eneo hilo la eka 3.5 halitoshi kujengwa stendi hiyo.

**d) Eneo inapotaka kujengwa stendi kuwa oevu**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imejulishwa kuwa eneo linalokusudiwa kujengwa stendi ni oevu. Maeneo oevu ni maeneo yanayoweza kunyonya maji ya mafuriko ya mvua na hivyo kuweza hupunguza mafuriko ya maji yanayotokana na

mvua. Kujenga stendi eneo hilo kutasababisha mafuriko ya maji ya mvua kuweza kuathiri makazi ya watu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeona kuwa eneo hilo la stendi linazungukwa na barabara za mitaa. Kamati imebaini kuwa ikiwa stendi hiyo itajengwa na kuzuia mtiririko wa maji yanayotokana na mvua kunaweza kutokea mafuriko yatakayoathri barabara za mitaa katika eneo hilo.

**e) Barabara zinazoingia eneo la Stendi kuwa nyembamba**

**Mheshimiwa Spika,** Upimaji wa ramani wa Mji wa Mikumi umetenga barabara zinazoingia eneo linakotakiwa kujengwa Stendi ya Mabasi Mikumi kuwa nyembamba. Sababu ya kusanifu barabara hizo kuwa nyembamba ni kutokana na barabara hizo nyingi kuwa ni barabara za mitaa. Hivyo, haikutarajiwa maeneo hayo kupitisha magari yenye uzito mkubwa. Stendi ya Mabasi Mikumi imepangwa kujengwa kwa madhumuni ya kupokea mabasi madogo na makubwa. Kutokana na hilo, Kamati inaona kuwa stendi hiyo haitakuwa na ufanisi kutokana na miundombinu ya barabara zinazoelekea itakapokuwa stendi kuwa finyu.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** baada ya uchambuzi wa masuala mbalimbali yaliyojitokeza wakati wa ukaguzi wa mradi huu Kamati inatoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo: -

(a) Kutokana na sintofahamu iliyobainika kwa Kamati kuhusu eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa mradi wa stendi ya mabasi ya Mikumi; Kamati inashauri Serikali itume timu ya uchunguzi eneo hilo ili kusimamia utengaji wa eneo la stendi ya mabasi kwa kuzingatia maslahi ya wananchi;

(b) Kamati inashauri eneo lililopo kati ya eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa stendi na eneo la wazi ambalo lina makazi ya wananchi litwaliwe kutoka kwa wananchi kwa kuwalipa fidia ili eneo hilo liwe sehemu ya eneo la Mamlaka ya Mji; na

(c) Kamati inashauri Halmashauri kutenga bajeti walau asilimia mbili (2%) kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya kimkakati ili kutokutegemea fedha kutoka Serikali Kuu pekee katika utekelezaji wa miradi.

2.1.2 **Utekelezaji wa Mradi wa Uboreshaji wa Barabara za Mikumi Mjini *(Upgrading of Mikumi Town Roads 1.45 km to Rigid Pavement in Kilosa District)* (Mradi Na. S01/014/2024/2025/W/73)**

**Mheshimiwa Spika,** Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa inatekeleza Mradi wa Uboreshaji wa Barabara za Mikumi Mjini kwa kujenga barabara yenye urefu wa Km. 1.45 kwa kiwango cha zege. Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi mzawa anayejulikana kama *Trinity Manufacturing Services Limited* ya Dar es Salaam; chini ya Wakala wa Barabara za Mijini na Vijijini (TARURA).

**Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Spika;** mradi huu utakapokamilika utarahisisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa na watu kutoka sokoni na maeneo ya machinjio, kuunganisha maeneo ya kulala watalii na hoteli, kuongeza thamani ya ardhi na makazi ikiwemo kuunganisha viwanja vipya zaidi ya 1,153 vya matumizi ya makazi, biashara, elimu na hoteli.

**Hatua za Utekelezaji wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** Mradi huu ulianza kutekelezwa mnamo tarehe 13/12/2024 kwa gharama ya shilingi 1,322,436,066.00 ambazo ni fedha za tozo ya mafuta. Mradi huu unatarajiwa kukamilika tarehe 12/05/2026. Hadi wakati Kamati inatembelea mradi huu kwa ajili ya ukaguzi ulikuwa umefikia asilimia 55 ya utekelezaji wake. Mradi unatarajia kukamilika tarehe 20 Aprili, 2026.

**Changamoto**

**Mheshimwa Spika,** wakati wa utekelezaji wake mradi huu umekumbana na changamoto kadhaa ikiwemo ucheleweshaji wa malipo ya awali *(Advance Payment),* mvua kubwa zilizonyesha Mkoani Morogoro pamoja na kuchelewa kwa msamaha wa kodi, hali iliyoathiri kasi ya utekelezaji wa mradi.

**Uchambuzi wa Kamati**

***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Barabara ya Mikumi Kamati ilifanya uchambuzi kuhusu na mradi huo. Katika uchambuzi wake Kamati imebaini masuala mbalimbali ya msingi kama ifuatavyo: -

**a) Kukosekana kwa mitaro**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ilibaini kuwa usanifu wa ujenzi wa barabara hiyo haukuhusisha ujenzi wa miundombinu kwa ajili ya mitaro pamoja na njia ya watembea kwa miguu.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inatambua kuwa kukosekana kwa mitaro kunaweza kusababisha uhai wa barabara hiyo kuwa mdogo kutokana na uwezekano wa maji ya mvua kusababisha mmomonyoko wa udongo.

**Mheshimiwa Spika,** barabara hiyo inapita katika makazi ya watu. Ni wazi kuwa wananchi watembea kwa miguu watakuwa wakiitumia barabara hiyo. Kukosekana kwa njia ya watembea kwa miguu pembezoni mwa Barabara hiyo kunaweza kukasababisha usumbufu, ama hata ajali kwa watembea kwa miguu.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

Kwa kuwa barabara hii inaelekea katika stendi ya mabasi na eneo la soko, Serikali iangalie namna ya kuiboresha ili iweze kumudu uzito wa magari unaoruhusu shughuli za kiuchumi.

### 2.1.3 Kuendeleza Ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Morogoro (Mradi Na. 3249)

***Mheshimiwa Spika***, Mradi wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro unatekelezwa katika Kata ya Kihonda Mtaa wa Nguvu Kazi.

**Mheshimiwa Spika**; Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Morogoro ulianza kutekelezwa kwa kutumia mfumo wa *force account* katika mwaka wa Fedha 2021/2022 ambapo hadi kukamilika kwake ulikadiriwa kutumia jumla ya **shilingi 7,000,000,000.00** kwa kujenga jumla ya majengo/miundombinu 28 ya Afya. Hadi kufikia muda wa ukaguzi wa Kamati, tayari fedha kiasi cha **shilingi 3,024,800,000.00**, kilikuwa kimeshatumika, ikiwa **shilingi 2,878,800,000.00** kutoka Serikali Kuu na **shilingi 146,000,000.00** kutoka mapato ya ndani ya Halmashauri.

**Hatua za Utekelezaji wa Mradi**

***Mheshimiwa Spika***; hadi kufikia wakati wa ukaguzi wa Kamati tayari majengo 13, ambayo ni Jengo la Wagonjwa wa Nje (OPD), Maabara, Jengo la mionzi (Radiology), Jengo la Upasuaji (Theatre), Wodi ya Wanawake, Wodi ya Wanaume, Wodi ya upasuaji Wanaume, Wodi ya kina Mama Wajawazito na Upasuaji *(Maternal Complex),* Wodi ya Watoto *(Pediatric),* Jengo la kuhifadhia miili *(Mortuary),* Jengo la kufulia, Jengo la kuhifadhia dawa *(Pharmacy)* na Nyumba ya Watumishi *(Three in one*) yalikuwa tayari yamekwishakamilika kwa asilimia 100.

**Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Spika**; kukamilika kwa mradi huu kumepelekea faida mbalimbali zikiwemo: -

i) Kutoa huduma za afya kwa wananchi wa Manispaa na maeneo ya Jirani; na
ii) Kuwa Kituo cha rufaa cha kutolea huduma za Afya kwa Vituo vya Afya na Zahanati zilizopo katika Manispaa ya Morogoro.

**Changamoto**

**Mheshimiwa Spika;** Kamati ilitaarifiwa kuwa wakati wa utekelezaji wa mradi huu hakukuwa na changamoto yoyote. **Kamati inatilia shaka taarifa hii.**

**Uchambuzi wa Kamati**

***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa ya utekelezaji wa mradi wa ujenzi wa Hospitali ya Manispaa ya Morogoro Kamati ilifanya uchambuzi wake kuhusu na mradi huo. Katika uchambuzi huo Kamati imebaini masuala mbalimbali ya msingi kama ifuatavyo: -

**a) Ujenzi kufanyika katika eneo oevu**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa eneo ilipojengwa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro ni oevu na linalokusanyika maji kutoka uwanda wa juu.

***Mheshimiwa Spika,*** utekelezaji wa mradi huu unaweza kusababisha maeneo ya jirani, ambako kuna makazi ya watu kukumbwa na mafuriko ya mvua ya mara kwa mara. Vilevile, Kamati imebaini kuwa, matenki ya maji taka yaliyojengwa maeneo hayo oevu yanaweza kujaa mara kwa mara na maji ya mafuriko. Hii inaweza kusababisha magonjwa ya mlipuko kwa wananchi.

**b) Ujenzi usiofuata utaratibu**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ilibaini kuwa majengo mengi yamekuwa yakitinduliwa kwa ajili ya kuweka miundombinu ya umeme na maji baada ya kupigwa plasta. Kamati inatambua kuwa ujenzi wa majengo ya Serikali hufuata utaalam; na katika hili Kamati ilifahamishwa kuwa kwa utaalam wa ujenzi, kabla ya kupiga plasta inawekwa miundombinu ya maji safi na maji taka pamoja na miundombinu ya umeme. Suala la kuweka miundombinu hiyo baada ya kupiga plasta ni kukosa weledi na utaalam. Ujenzi huu usioufuata utaalam na taratibu za ujenzi unaweza kusababisha athari kubwa na kuleta hasara kwa Serikali.

**c) Usimamizi hafifu wa mradi**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa mradi huu unatumia *force account,* hivyo mafundi wanaotekeleza mradi huu ni mafundi wasio na elimu ya uhandisi wa darasani *(local fundi)*. Mafundi hawa huhitaji usimamizi wa karibu ili kuhakikisha kuwa wanaelekezwa kuhusu viwango vya ujenzi vinavyohitajika katika utekelezaji wa mradi. Kamati imebaini kasoro kadha wa kadha zilizosababisha kuleta hisia kuwa wataalam wa Halmashauri hawakuwa makini katika usimamizi wa mradi huu.

**d) Ujenzi kutokufuata BOQ**

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa mbao zilizotumika kwa ajili ya kupaua katika baadhi ya majengo iliyoyakagua, hasa kwenye njia za kupitia kuunganisha majengo *(walkways)* ni za kawaida ilihali *BOQ* inataka mbao za kupaua majengo ziwe *treated*. Hii inaonesha kuwa kulikuwa na udhaifu kwa upande wa manunuzi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

(a) Kamati inashauri Serikali kuimarisha usimamizi na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi. Wakuu wa Idara na Vitengo watekeleze majukumu yao ipasavyo pamoja na kushughulikia dosari zote zilizobainika kwenye mradi;

(b) Serikali kupitia OWM- TAMISEMI iendelee kusisitiza Halmashauri kufuata ramani, michoro na miongozo inayotolewa na OWM-TAMISEMI katika utekelezaji wa miradi ya ujenzi ili miradi hiyo itekelezwe kwa ufanisi na kuleta tija iliyokusudiwa kwa wananchi;

(c) Serikali ifanye msawazo wa watumishi wa afya na kuendelea kutenga ikama itakayowezesha kuajiri wataalamu wa afya 113 wanaohitajika katika hospitali ya Manispaa Morogoro ili kuwezesha kupatikana kwa huduma zote muhimu kwa wananchi; na

(d) Kwa kuwa Serikali iliomba kuongezewa muda wa kukamilisha mradi huu hadi tarehe 15 Mei, 2026, Kamati inasisitiza Serikali kuhakikisha kuwa mradi unakamilika ndani ya muda huo na

katika ubora unaotakiwa ili kutoa huduma zilizokusudiwa kwa wananchi.

### 2.1.4 Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji kwa ushindani Manispaa ya Morogoro (Mradi LGA/079/2022/2023/HQ/W/16/PCKG/01)

**Mheshimiwa Spika,** Mradi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Miji *(Tanzania Cities Transforming Infrastructures and Competitiveness Project)* kwa ushindani unatekelezwa na Serikali kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI kwa fedha za mkopo kutoka Benki ya Dunia, ukiwa na lengo la kuboresha miundombinu ya miji, manispaa na majiji.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilikagua miradi iliyo sehemu ya utekelezaji wa mradi huo inayotekelezwa katika Mkoa wa Morogoro. Katika mkoa huo Kamati ilikagua ujenzi wa Barabara ya Muhimbili (1.2km) ambayo utekelezaji wake ulifanyika katika Awamu ya Kwanza *(TACTIC Package 1)* na ulishakamilika kwa asilimia 90.9 pamoja na mradi wa Ujenzi wa Stendi ya Mabasi Madogo Kihonda, ambao unatekelezwa katika Awamu ya Pili *(Package 2)*.

***Mheshimiwa Spika***; mradi huu unatekelezwa kwenye eneo lenye mita za mraba 55,723.32, na unatekelezwa na Mkandarasi M/S TIL Construction Limited kwa gharama ya shilingi 13,460,689,504.61 na kusimamiwa na Mhandisi Mshauri M/S Mhandisi Consultancy Limited akishirikiana na M/S CORE Consulting Engineers PLC kwa gharama ya Shilingi 1,743,927,140.00.

**Hatua za Utekelezaji:**

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ni wa muda wa miezi 12, kuanzia tarehe 21/07/2025 hadi tarehe 21/07/2026. Hadi kufikia wakati wa ukaguzi wa Kamati mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 52 ya utekelezaji.

**Faida za Mradi**

***Mheshimiwa Mwenyekiti,*** kukamilika kwa mradi huu wa ujenzi wa stendi kutaleta manufaa yafuatayo: -

i) Kuboresha mazingira ya usafiri na usafirishaji hususani kwa wananchi wanaotumia usafiri wa reri ya kisasa, ambao watapata eneo rasmi la kupata usafiri wa kuelekea maeneo mbalimbali ndani ya Manispaa ya Morogoro;

ii) Kurahisisha huduma ya usafiri na usafirishaji kwa wananchi wa maeneo ya Kata ya Kihonda na Kata za jirani;

iii) Kuwepo kwa ajira za moja kwa moja kwa wananchi ambao wataendesha biashara zao ndani ya stendi hii; na

iv) Kuongeza makusanyo ya Halmashauri.

**Uchambuzi wa Kamati**

**Ubora wa Barabara**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa Barabara ya Muhimbili imejengwa kwa ubora. Kamati inaipongeza Serikali kwa utekelezaji wa mradi huu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imebaini kuwa barabara hii ndiyo Barabara ya kwanza ya mzunguko katika Manispaa ya Morogoro iliyo mchepuko *(bypass)* ya Barabara ya Dar es Salaam Kwenda Dodoma bila kupitia maeneo ya mjini. Kamati inaona kuwa barabara hii ni ya muhimu sana kwa kuwa itapunguza foleni iliyoko katika Barabara ya Dar es Salaam kuanzia maeneo ya Njiapanda ya Kihonda – VETA, Mzunguko *(roundabout)* wa Msamvu hadi Nanenane. Kamati inaipongeza TARURA na Serikali kwa ujumla kwa usanifu wa barabara hii.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i) Kwa kuwa mradi ulisanifiwa bila kuweka eneo kwa ajili ya maegesho ya magari madogo, Kamati inashauri kuwa Serikali iangalie uwezekano wa kutenga eneo kwa ajili ya kuegesha magari madogo;
ii) Serikali ihakikishe kuwa inatenga bajeti kwa mwaka wa fedha 2026/2027 ili ikamilike kwa wakati ili kusaidia kupunguza foleni Katikati ya Mji wa Morogoro.

### 2.1.5 Ujenzi wa Barabara ya Picha ya Ndege – Bokotimiza (0.52km) kwa kiwango cha lami

**Mheshimiwa Spika**, Barabara ya Picha ya Ndege - Bokotimiza yenye urefu wa kilomita (0.52km) utekelezaji wake umeanzia kwenye makutano ya Barabara ya Morogoro na kupitia maeneo muhimu ikiwemo magereza, hospitali na shule kabla ya kufika eneo la Bokotimiza kwa urefu wa kilometa 7.88.

**Faida za Mradi**

**Mheshimiwa Spika**, kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuborehsa usafiri wa watu na usafirishaji wa miradi katika eneo hilo na hivyo kukuza uchumi na kuleta ustawi kwa wananchi wanaoishi karibu na wanaotumia barabara hiyo.

**Uchambuzi wa Kamati**

**a) Barabara kutokuwa na stendi za mabasi *(bus bay)***

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Barabara ya Picha ya Ndege – Bokotimiza haina maeneo ya kusimama magari *(bus bay)*. Pamoja na magari mengine kupita katika barabara hiyo, barabara hiyo pia itatumiwa na vyombo vya usafiri wa umma kama mabasi ya abiria, daladala na bajaji.

***Mheshimiwa Spika,*** kukosekana kwa maeneo ya kusimama mabasi *(bus bay)* kutasababisha magari ya abiria

yatakayokuwa yanapita katika barabara hii kukosa mahala pa kusimama kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria. Hali hii inaweza kusababisha magari ya aina hiyo kusimama Katikati ya barabara, hali inayoweza kusababisha ajali na foleni.

**b) Barabara kutokuwa na taa za barabarani**

***Mheshimiwa Spika,*** ni utaratibu uliowekwa na Serikali kuhakikisha kuwa barabara zote zinazojengwa, zikipita katika makazi ya watu kusimikwe taa za barabarani.

***Mheshimiwa Spika,*** wakati wa ukaguzi wa barabara hii Kamati imebaini kuwa hakuna taa za barabarani zilizosimikwa katika vipande vya barabara vilivyojengwa huku vikiwa vimekamilika kwa asilimia 100.

**c) Barabara kujengwa vipande vifupivifupi kwa mita zisizozidi 600 kila mwaka,**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati imebaini kuwa barabara hii inajengwa kwa vipande vya wastani wa mita 500 kila mwaka.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati imetaarifiwa kuwa barabara hii inajengwa kutoka Picha ya Ndege hadi Bokotimiza, ambapo inagusa hadi katika stesheni ya SGR ya Soga, ( 7.8km). Hivyo Kamati inaona kuwa barabara hii ni muhimu kwa kuwa inawezesha wasafiri wanaotumia usafiri wa treni ya SGR kwenda na kurudi Morogoro, Dodoma, na Dar es Salaam.

***Mheshimiwa Spika,*** katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa, ikiwa Barabara hii itaendelea kujengwa kwa vipande vya mita 500 kila mwaka itachukua miaka takriban 12 ili kuikamilisha. Hali hii inaweza kupoteza umaana na umuhimu wa barabara hii. Aidha, inawezekana kabisa kabla barabara kuanza kuharibika kabla haijakamilika.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

(a) Kamati inashauri Serikali kutenga bajeti ya kujenga kipande chote cha barabara kilichobaki kwa changarawe ili ianze kutumika wakati bajeti ya kujenga kwa lami inaendelea kutengwa;

(b) Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya makaravati na mitaro inaelekeza maji karibu na makazi ya watu kabla ya kufika kwenye mkondo uliokusudiwa na hivyo kuweza kusababisha mafuriko kwenye makazi ya watu. Kamati inashauri mitaro hii kurefushwa ili kuondoa uwezekano wa mafuriko kwenye makazi ya watu;

(c) Kamati inashauri Serikali kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kujumuisha uwekaji wa taa za barabarani katika miradi yote ya ujenzi wa barabara.

### 2.1.6 Ujenzi wa Barabara ya Kongowe – Forest – Yombo (0.7km) kwa kiwango cha Lami.

**Mheshimiwa Spika,** utekelezaji wa mradi huu ulianza rasmi tarehe 21 Novemba, 2024 na unatarajiwa kukamilika tarehe 04 Mei, 2026. Hadi kufikia kipindi cha ukaguzi wa mradi tayari mkandarasi alikuwa ameshalipwa jumla ya shilingi 661,849,315.00 na kazi ilikuwa imefikia asilimia 95 ya utekelezaji wake.

**Faida ya Mradi**

**Mheshimiwa Mwenyekiti;** Kukamilika kwa ujenzi wa Barabara hii ambayo inaanzia kwenye makutano ya Barabara ya Morogoro na inapitia kwenye maeneo muhimu ikiwemo Ofisi za Misitu (TFS), Hosptali na Shule kabla ya kufika eneo la Yombo kwa urefu wa kilomita 19.69**,** pamoja na kuwa ni kiungo muhimu kati ya Wilaya ya Kibaha na Bagamoyo, ina umuhimu mkubwa katika kuimarisha maendeleo ya jamii na ukuaji wa uchumi, itarahisisha usafiri wa watu na bidhaa, itaboresha upatikanaji wa huduma za afya na elimu, na inachochea shughuli za kibiashara na uzalishaji.

**Uchambuzi wa Kamati**

***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kongowe – Forest – Yombo, pamoja na kufanya ukaguzi, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu taarifa hiyo. Katika uchambuzi huo Kamati imebaini masuala mbalimbali ya msingi kama ifuatavyo: -

**a) Kutokuwepo kwa mabamba *(slabs)* ya kutosha kuelekea katika makazi ya wananchi**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ilibaini kuwa Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya Kongowe – Forest – Yombo hauna mabamba *(Slabs)* ya kutosha kutoka barabarani kwenda katika makazi ya wananchi. Aidha, Kamati imeona mitaro iliyowekwa kwa ajili ya kupitisha maji ya mvua kwa ajili ya kulinda barabara kuwa inawazuia wananchi kutekeleza majukumu yao kwa urahisi.

***Mheshimiwa Spika,*** pembeni mwa barabara hii kuna makazi ya wananchi. Aidha, katika makazi hayo imebainika kuwa kuna shughuli mbalimbali kama vile biashara zinazoendelea.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

i) Serikali iendelee kutenga fedha ili barabara hii iweze kukamilika kwa wakati na kuleta tija iliyokusudiwa;

ii) Kamati inashauri Serikali kuongeza vivuko vya kuingia maeneo ya wananchi na maeneo yao ya kiuchumi (*slabs*) katika ujenzi wa barabara hii. Aidha, ujenzi wa barabara uende sambamba na kuweka njia au matoleo ya miundombinu mengine kama vile maji na umeme; na

### 2.1.7 Ujenzi wa Barabara ya Bomang'ombe – Kikavuchini kwa kiwango cha Lami (3.5km) (Mradi Na. S10/009/2023/2024/W/229)

**Mheshimiwa Spika;** mradi wa ujenzi wa Barabara ya Bomangómbe – Kikavuchini kwa kiwango cha lami *(Double Surface Dressing)* yenye urefu wa Km 25.7 ambayo inaanzia Bomangómbe hadi TPC una gharama ya shilingi 2,999,000,000.00. utaratibu wa ujenzi wa mradi huu ni kujengwa kwa awamu kadri ya upatikanaji wa fedha.

**Faida za Mradi**

**Mheshimiwa Spika;** baada ya kukamilika kwa mradi huo kutakuwa na faiida kama ifuatavyo: -

i) kutafungua fursa mpya na kukuza shughuli za utalii katika eneo la kivutio cha Chemka Hotspring;

ii) itakuwa njia mbadala wa Barabara kuu ya Arusha – Njiapanda ya Himo;

iii) itarahisisha usafiri wa watu na mizigo kuelekea katika mashamba ya TPC, Chuo cha Ufundi Arusha (ATC – Kikuletwa Campus), Chuo cha Ufundi VETA, Chuo cha Afya na Ualimu Mongáre; na

iv) Kuunganisha kata za Bomangómbe, Bongeni na Weruweru.

**Uchambuzi wa Kamati**

***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Barabara ya hii (3.5km), pamoja na kufanya ukaguzi, Kamati ilibaini kuwa Barabara ya Bomang'ombe Kikavuchini ni barabara inayozifikia taasisi mbalimbali za umma na binafsi, ambazo ni; Chuo cha Ufundi Arusha *(Arusha Technical College),* Chuo cha Ualimu Mangare (Mangare Teachers College, Kituo cha Mafunzo ya Ufundi, pamoja na Kiwanda cha Sukari cha TPC.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitaarifiwa kuwa barabara hii imetolewa agizo na Mheshimiwa Waziri Mkuu kuhama kutoka TARURA na kwenda TANROADS. Kamati inapongeza uamuzi huu.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa barabara hii imewekwa vivuko (mabamba) vya kutosha kwa ajili ya kuwawezesha wananchi kuyafikia makazi yao. Kamati inapongeza jambo hili kwa kuwa litarahisisha wananchi kuendelea na shughuli zao bila usumbufu wowote.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

(a) Kamati inashauri ujenzi wa barabara hii uendelee wakati taratibu za kutekeleza maelekezo ya Mheshimiwa Waziri Mkuu ya kuhamisha mradi wa barabara hii kutoka TARURA kwenda TANROADS zinafuatwa ili kuwezesha wananchi kupata huduma iliyokusudiwa; na

(b) Kamati inashauri Serikali ihakikishe kwamba barabara zinazojengwa maeneo mbalimbali nchini zinawekwa vivuko vya vya kutosha kwa ajili ya wananchi kuvitumia ili kuingia katika maeneo yao, na kuweka matoleo ya kuwezesha kujengwa miundombinu mingine itakayohitajika.

### 2.1.8 Ujenzi wa Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia (Mradi Na. 4390)

**Mheshimiwa Spika;** mradi wa ujenzi wa Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia ambao umeanzishwa kwa lengo la kuboresha mazingira bora ya ufundishaji na ujifunzaji katika shule za sekondari na pia kuongeza idadi ya Shule za Sekondari katika wilaya ya Longido, umetekelezwa kwenye Kata ya Orbomba Kijiji cha Oltepes. Shule hii ni mojawapo ya Shule 26 zilizojengwa Tanzania nzima chini ya uongozi wa Dkt. Samia Suluhu Hassan Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika jitihada zake za kuelimisha na kuendeleza jamii ya Tanzania hasa Watoto wa kike. Shule hii ambayo ina usajili wa wa S.6575 ilianza kutekeleza

majukumu yake mnamo tarehe 01/07/2024 ikiwa na Wanafunzi wa kidato cha tano ikiwa na michepuo ya sayansi (PCB, PCM na CBN).

***Mheshimiwa Spika***; Mradi wa Ujenzi wa shule ya Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia umetekelezwa kwa fedha kiasi cha Shilingi 4,450,000,000.00 ambapo utekelezaji wake umefanywa katika Awamu 3.

**Changamoto**

***Mheshimiwa Spika***; wakati wa ukaguzi wa Kamati ilielezwa kuwa mradi huu wakati wa utekelezaji wake ulikumbana na changamoto za upandaji wa gharama za vifaa vya ujenzi tofauti na fedha zilizopokelewa awali, kuwepo kwa tofauti kati ya fedha zilizopokelewa na gharama halisi za mradi ukilinganisha na mwongozo wa TAMISEMI na kuwepo kwa ongezeko (*variation*) ya idadi ya malighafi/vifaa vilivyohitajika kweney ujenzi.

**Uchambuzi wa Kamati**

***Mheshimiwa Spika,*** baada ya kupokea taarifa ya Wizara kuhusu utekelezaji wa Mradi wa Ujenzi wa Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia pamoja na kufanya ukaguzi, Kamati ilifanya uchambuzi wa kina kuhusu mradi huu. Katika uchambuzi wake Kamati imebaini mambo mbalimbali ya msingi kama ifuatavyo: -

a) **Uwepo wa nyufa nyingi katika baadhi ya majengo**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati ilibaini kuwa katika majengo kadhaa yaliyokaguliwa na Kamati kuna nyufa katika baadhi ya kuta. Uwepo wa nyufa hizi unaweza kusababisha madhara makubwa kwa kuta hapo baadaye.

b) **Kubanduka kwa rangi za kuta za nje katika baadhi ya majengo**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati pia imebaini kuna baadhi ya majengo rangi yake imeanza kubanduka katika maeneo mengi. Hali hii inaweza kusababishwa na ubora mdogo wa rangi iliyotumika, umakini mdogo wakati wa ujenzi, na, ama

usimamizi mdogo. Aidha, ikiwa kuta hizo zitaendelea kuachwa bila kushughulikiwa kuna uwezekano wa tatizo hili kukua.

**c) Matumizi ya milango ya mabati**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati imebaini kuwa kuna baadhi ya majengo, kama vile maabara na bwalo milango iliyowekwa ni ya bati gumu. Kamati ilitaka kujua ikiwa matumizi ya milango hiyo ni maelekezo ya Wizara. Katika majibu yake Wizara imesema kuwa maelekezo ya Wizara ni kutumia mbao ngumu au malighafi inayofanana na hiyo. Kamati inafahamu kuwa malighafi ya bati si malighafi inayofanana na malighafi ya aina ya mbao.

***Mheshimiwa Spika,*** hata hivyo Kamati imetaka kujua ubora, madhara, na umaridadi wa matumizi ya milango ya bati. Kamati ilijibiwa kuwa milango hiyo haina shida kubwa. Kamati imebaini kuwa kati ya shule zote na mejengo yote ya Serikali yaliyokaguliwa na Kamati mradi huu ni wa kwanza kuwa na milango ya aina hiyo. Kamati ilitaka kujua sababu za matumizi ya milango hiyo, na kwa nini isiwe milango ya mbao na kujibiwa kuwa ni kutokana na changamoto ya upatikanaji wa malighafi za mbao.

***Mheshimiwa Spika,*** katika uchunguzi wake Kamati imeng'amua kuwa matumizi ya milango ya mabati katika majengo ya Serikali haina kiwango kizuri kwa mwonekano na hakuyafanyi majengo kuwa maridadi.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa kina na kubaini kuwa milango ya mabati ina gharama nafuu zaidi ya milango ya mbao. Aidha, upatikanaji wa milango ya bati ni rahisi zaidi kuliko milango ya mbao. Vilevile, Kamati imebaini kuwa milango ya mbao huongeza thamani ya jengo na kulifanya jengo kuwa maridadi na bora zaidi.

**d) Utofauti wa viwango vya magodoro ya wanafunzi katika mabweni**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati imebaini kuwa magodoro wanayoyatumia wanafunzi wa shule hii yana viwango tofautitofauti. Kamati ilitaka kufahamu sababu ya viwango hivi kutofautiana na kujibiwa kuwa ni kutokana na wanafunzi kuagizwa kuja na magodoro yao.

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati inafahamu kuwa utofauti wowote wa kimsingi *(basic difference)* kati ya wanafunzi huweza kusababisha hisia za unyonge kwa baadhi ya wanafunzi. Hali hii huweza kuathiri uwezo wa mwanafunzi aliyeathirika kutokufanya vizuri katika masomo yake.

**e) Fedha za ujenzi kutokutosha**

***Mheshimiwa Spika,*** katika uchambuzi wa mradi huu, Kamati imebaini kuwa majengo ya mabweni manne yanayojengwa hayajakamilika ilihali fedha kwa ajili ya ujenzi wa mabweni hayo imekwisha. Kamati iliuliza kutaka kujua sababu ya fedha kutokutosha na kujibiwa kuwa fedha zilizopangwa kwa ajili ya majengo hayo hazikutumika zote kwa kuwa sehemu ya fedha hizo zilitumika kwa ajili ya kumalizia majengo ya nyuma ambayo pia fedha zake hazikutosha. Kamati ilitaka kujua ikiwa wametumia utaratibu kuhamisha fedha hizo na kujibiwa kuwa wametumia utaratibu wa kawaida wa kuhamisha fedha *(funds reallocations)*. Hali hii imekuwa ikisababisha usumbufu wa kuomba fedha kidogo kidogo.

**f) Ofisi ya RAS kutenga bajeti kwa ajili ya kuajiri maafisa milki kwenye shule za kimkakati**

Wakati wa uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa uwepo wa uchakavu wa majengo pamoja na nyufa mbalimbali kunahitajika kuwe na afisa atakayesimamia utunzaji wa majengo. Kutokuwepo kwa mtu wa kusimamia majengo kunafanya kusiwepo na mtu wa kuyatazama majengo na kumshauri mwenye mamlaka kuhusiana

na namna bora ya kutunza majengo, lakini pia namna bora ya kufanya matengenezo mbalimbali ya kawaida.

**g) Kutokuwepo kwa uzio**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa katika shule hii ambayo ni moja ya shule za kimkakati haina uzio kwa ajili ya ulinzi wa wanafunzi. Kamati inatambua kuwa eneo hili la Longido ni eneo ambalo linazungukwa na mbuga zenye wanyamapori wengi zaidi.

**Mheshimiwa Spika,** shule hii ya Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia iko kwenye hatari kubwa kwa watoto wanaosoma shule hii kushambuliwa na wanyamapori. Kukosekana kwa uzio katika shule hii kunasababisha wanafunzi kuishi kwa hofu ya wanyamapori wakali. Hali hii inaweza ikaleta shida ya kisaikolojia na hivyo kuweza kusababisha kushuka kwa kiufanisi katika masomo yao.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

(a) Kamati inashauri Serikali kuimarisha usimamizi wa ndani ya shule pamoja na shule kufanyiwa matengenezo ya mara kwa mara (*routine maintenance*) ili kuongeza muda wa matumizi wa mali za shule na kuepusha kutumia gharama kubwa baadaye katika matengenezo ya miundombinu ya shule;

(b) Kamati inashauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa shule ili kulinda usalama wa wanafunzi dhidi ya Wanyama wa porini, kulinda miundombinu ya shule lakini pia ili kudhibiti mienendo ya wanafunzi.

### 2.1.9 Ujenzi wa Shule Mpya ya Msingi ya Mkondo Mmoja - Shule ya Msingi Lowasa (Mradi Na. 4312)

***Mheshimiwa Spika,*** katika ukaguzi wake Kamati ilitembelea na kukagua mradi wa Ujenzi wa Shule Mpya ya Msingi ya Mkondo mmoja, ambao unatekelezwa na Serikali kupitia mradi wa *BOOST*.

Mradi huu ulianza kutekelezwa rasmi tarehe 04/09/2024 na ulitarajiwa kukamilika tarehe 30/03/2026.

**Faida ya Mradi**

***Mheshimiwa Spika***; kukamilika kwa mradi huu pamoja na kuwezesha wanafunzi kupata mazingira mazuri na rafiki ya kujifunzia pia utasaidia kuongeza idadi ya shule za msingi katika Halmashauri ya Wilaya ya Longido kutoka shule 99 zilizopo na kufikia shule 100, kuondoa msongamano madarasani na kupandisha kiwango cha udahili wa wanafunzi wa awali na wa msingi kila mwaka.

**Uchambuzi wa Kamati**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati baada ya kuutembelea, kupokea taarifa na kuukagua Mradi wa Ujenzi wa Shule hii, ilifanya uchambuzi wake ili kufahamu ikiwa mradi huu umetekelezwa kama ilivyokusudiwa. Katika uchambuzi wake Kamati ilibaini masuala mbalimbali kama ifuatavyo: -

**a) Kutofautiana kwa ramani za majengo**

***Mheshimiwa Spika,*** wakati Kamati ikichambua kuhusu utekelezaji wa mradi huu ilibaini kuwa kuna utofauti wa ramani za majengo kati ya jengo moja na lingine. Kamati imebaini kuwa utofauti wa ramani hizo umesababisha pia kuonesha utofauti katika ubora wa majengo. Kamati inaamini kuwa ujenzi wa majengo ya shule za Serikali hufuata mitindo inayofanana ili kuyafanya kuwa bora na maridadi, imara na ya kuvutia. Kamati haikupendezwa na utaratibu wa ujenzi wa majengo haya kutofautiana.

**b) Ujenzi usiofuata utaratibu**

***Mheshimiwa Spika,*** Kamati imebaini kuwa ujenzi wa shule hii haukufuata utaratibu. Hii ni kutokana na Kamati kugundua kuwa kuna miundombinu ya maji safi na maji taka iliyojengwa baada ya majengo kupigwa plasta. Hali inaonesha kuwa aidha kuna uzembe kwa mafundi waliojenga jengo hilo, au mafundi waliojenga hawana ujuzi katika mambo ya ujenzi, au hapakuwa na usimamizi wa kutosha kutoka kwenye mamlaka za usimamizi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

(a) Kamati inashauri Serikali kuhakikisha shule hii inatengewa fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio wa shule ili kulinda usalama wa wanafunzi dhidi ya wanyama wa porini, kulinda miundombinu ya shule lakini pia kudhibiti mienendo ya wanafunzi;

(b) Serikali ihakikishe shule ijengwa mabweni kwa ajili ya wanafunzi ili kulinda usalama wa wanafunzi watakaotakiwa kutembea umbali mrefu kufika shuleni lakini pia kuwezesha wanafunzi hao kupata elimu pale ambapo familia zao za kifugaji zitakapokua zinahama; na

### 2.1.10 Ujenzi wa Sekondari ya Migungani (Mradi Na. 4390)

**Mheshimiwa Spika,** mradi wa ujenzi wa Shule ya Sekondari Migungani One umetekelezwa kwenye Halmashauri ya Monduli kupitia Shule mama ya Sekondari Manyara. Mradi huu ulianza kutekelezwa kuanzia mwaka wa fedha 2020/2021 na ulikamilika katika mwaka wa fedha 2024/2025, ukiwa na gharama ya Shilingi 882,158,029.

**Hatua za Utekelezaji wa Mradi**

***Mheshimiwa Spika***; mpaka kufikia wakati wa ukaguzi wa Kamati, mradi huu ulikuwa umekamilika na majengo mengi yameshaanza kutumika, isipokuwa madarasa mawili yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi, ambayo Kamati ilielezwa kuwa yataendelea kukamilishwa kulingana na upatikanaji wa fedha.

**Faida za Mradi**

***Mheshimiwa Spika;*** uwepo wa mradi huu kumesaidia kupunguza mlundikano wa wanafunzi katika shule za sekondari zilizo ndani ya Halmashauri. Vilevile umeogeza idadi ya shule zilizo ndani ya Halmashauri ya Monduli kutoka shule 27 hadi kufikia shule 28.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

(a) Kamati inashauri Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya kumalizia maboma mawili ya madarasa yaliyojengwa kwa nguvu za wananchi ili madarasa hayo yaweze kukamilika na kutumika na tija iliyokusudiwa iweze kupatikana;

(b) Kamati inashauri Halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika Shule ya Sekondari Migungani One ili kulinda usalama wa wanafunzi dhidi ya wanayama wa porini; na

(c) Kamati inashauri Serikali kutenga fedha kwa ajili ya ujenzi wa bwalo la wanafunzi kula chakula ili kuwezesha wanafunzi hao kula katika mazingira bora na kuzuia mlipuko wa magonjwa yanayoweza kutokea.

2.1.11 **Ujenzi** wa Kituo Kikuu cha Mabasi yaendayo Mikoani (*Bondeni City Bus Terminal*)

(Mradi Na. 7003/TACTIC/P171189/2024-2025/W/01)

***Mheshimiwa Spika***; mradi wa ujenzi wa Kituo Kikuu cha Mabasi (*Bondeni City Bus Terminal*) unatekelezwa na Kampuni ya M/S MOHAMMED BUILDERS LIMITED kwa gharama ya Shilingi 14,317,331,493.00 na unasimamiwa na Mhandisi Mshauri kutoka kampuni ya Mhandisi Consultancy Ltd kwa ushirikiano na kampuni ya GBS Consultant Ltd za Dar es Salaam.

***Mheshimiwa Spika***, muda utekelezaji wake ulikadiriwa kuwa ni wa mwaka mmoja, kuanzia tarehe **30/05/2025 hadi tarehe 30/05/2026**. Mradi umesanifiwa kuwa na miundombinu mbalimbali ikiwemo sakafu ya chini yenye ukubwa wa mita za mraba 8,400, sakafu ya pili yenye ukubwa wa mita za mraba 2,575, maeneo ya maegesho ya magari, vyumba vya biashara 46, maliwato za jinsia zote 2, maliwato za watu wenye mahitaji maalum, vyumba viwili vya ibada kwa Dini za Kiislamu a Kikristo, vyumba 80 vya kulala (Hostel) kwa wasafiri wanaohitaji kupumzika, Kituo cha Polisi, miundombinu rafiki kwa wazee na watu wenye ulemavu kuweza kufikia maeneo yote ya jengo ikiwa ni pamoja na sakafu za juu, vyumba maalumu kwa ajili ya ofisa wa uhamiaji, Idara ya Uokoaji na Zima Moto na

miundombinu okozi wakati wa dharura ikiwemo moto, Matetemeko na vingineyo. Hadi kufikia kipindi cha ukaguzi wa Kamati mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 70.96% ya utekelezaji wake na mkandarasi alikuwa ameshalipwa fedha kiasi cha Shilingi 2,564,307,482.00 sawa na asilimia 17.91 ya gharama za mradi.

**Changamoto**

***Mheshimiwa Spika***; wakati wa ukaguzi wa mradi Kamati ilielezwa kuwa utekelezaji wa mradi huu ulikuwa umekumbana na changamoto mbali mbali ambazo zilimchelewesha Mkandarasi kuweza kufikia malengo yake kwa kiasi cha asilimia kumi na nne (**14%**) na kufanya Mkandarasi kuomba na kukubaliwa kuongezewa muda wa miezi sita ili kukamilisha kazi hiyo. Miongoni mwa changamogo hizo ni pamoa na: -

a) Eneo lililosanifiwa awali liligundulika kuingiliana na miundombinu ya umeme mkubwa, hivyo ikalazimika kusogeza majengo upande mwingine wa eneo lilipo mradi sasa; na
b) Uwepo wa tabaka la udongo usiofaa kwa ujenzi *(black cotton soil)* ambapo kwa maelekezo ya mhandisi mshauri, ililazimu kuondoa tabaka lote kabla ya kuanza Msingi wa ujenzi wa kituo.

**Uchambuzi wa Kamati**

**a) Uwepo wa vyumba vya kulala katika eneo la stendi**

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake Kamati imebaini kuwa Stendi hii, pamoja na huduma nyingine itakazotoa lakini pia itatoa huduma ya uwepo wa vyumba vya kulala kwa ajili ya wageni. Kamati inapongeza ubunifu huo. Hata hivyo, Kamati imetilia shaka ikiwa vyumba hivyo vitaweza kuleta faida kwa halmashauri kutokana na uzoefu uliopo wa kutokufanya vizuri kwa vyumba vya hote

katika maeneo yenye vyumba vya aina hiyo, kama vile Stendi Kuu ya Mabasi ya Mkoa wa Iringa.

**b) Kutokumaliza shughuli za ujenzi kwa muda uliopangwa**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa mradi huu ulipaswa kumalizika tarehe 30 Mei, 2026. Hata hivyo mradi umeongezewa miezi mingine sita ili kukamilisha ujenzi wake. Ucheleweshwaji wa kukamilika kwa mradi huo umetokana na eneo lililopaswa kujengwa stendi hiyo kupitiwa na njia kubwa ya umeme. Kamati ilitaka kujua ni kwa nini mkoa usingehamisha umeme huo badala ya kusanifu upya majengo katika eneo jipya. Kamati ilijibiwa kuwa baada ya kufanya upembuzi wa kina ilionekana kuwa ni rahisi kufanya usanifu upya kuliko kuhamisha nguzo na njia hizo za umeme.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imeendelea kubaini kuwa changamoto hiyo imetokana na ukosefu wa umakini wakati wa usanifu wa awali.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

(a) Serikali ihakikishe inaimarisha usimamizi wa mradi na unakamilika kwa wakati ili kutoa huduma iliyokusudiwa kwa wananchi;

(b) Kwa kuwa ujenzi wa Kituo Kikuu cha mabasi yaendayo mkoani ni mradi wa kimkakati, Serikali iangalie uwezekano wa kupata wawekezaji katika stendi hiyo ili kuongeza mapato ya halmashauri; na

### 2.1.12 Ujenzi wa Soko la kwa Mrombo

***Mheshimiwa Spika*;** Mradi wa Ujenzi wa Soko la kwa Mrombo, unatekelezwa katika eneo lenye mita za mraba 3,682, ambapo jumla ya eneo litakalojengwa ni mita za mraba 7,260 ukihusisha uboreshaji wa mazingira ya nje *(landscaping),* mifumo ya maji ya

mvua, maji taka, pamoja na miundombinu ya kisasa ya maegesho ya magari na vyombo vingine vya moto.

***Mheshimiwa Spika***; Mradi huu unaotekelezwa kwa gharama ya Shilingi 2,286,643,323.00, unatekelezwa na Kampuni ya **M/S MOHAMMED BUILDERS LIMITED** na unasimamiwa na Mhandisi Mshauri kutoka kampuni ya **Mhandisi Consultancy Ltd** kwa ushirikiano na kampuni ya **GBS Consultant** Ltd za Dar es Salaam.

**Faida za Mradi**

***Mheshimiwa Spika***; mradi huu utakapokamilika utawapatia wananchi wa eneo la mradi na maeneo Jirani faida mbalimbali zikiwemo: -

a) Ongezeko la wateja wa hali ya chini, kati na juu;
b) Kuongeza kipato cha maafisa usafirishaji (madereva wa bodaboda na bajaji); na

**Changamoto**

***Mheshimiwa Spika,*** mradi huu ambao awali ulipangwa kutekelezwa katika kipindi cha mwaka mmoja (**30/05/2025 – 30/05/2026**) utekelezaji wake ulichelewa kwa takribani miezi mitatu ili kutoa muda wa kufanya mapitio ya usanifu *(design review)* pamoja na maboresho ya michoro ya mradi, kulikotokana na ufinyu wa eneo lililotengwa kwa ajili ya ujenzi wa soko. Hadi kufikia kipindi cha ukaguzi wa Kamati mradi huu ulikuwa umefikia asilimia 53.79% ya utekelezaji wake na tayari Mkandarasi alikuwa ameshalipwa asilimia 30% ya gharama za mradi sawa na Shilingi 692,607,264/=.

**Uchambuzi wa Kamati kuhusu Mradi**

**a) Ujenzi wa soko kutokuzingatia uwepo wa stoo katika jengo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa ujenzi wa Soko la Kwa Mrombo haukuzingatia uwepo wa stoo kwa ajili ya kuhifadhia nafaka. Kamati inafahamu kuwa soko hili, pamoja na bidhaa nyingine itakuwa na wafanyabiashara watakaokuwa wanauza

nafaka, kama vile mahindi, mchele, maharage na vinavyofanana na hivyo. Kamati inaona kuwa kutokuwepo kwa miundombinu ya stoo kunaweza kusababisha usumbufu kwa wafanyabiashara.

**b) Baadhi ya maeneo yanayopakana na soko kuwa katika hali duni**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa kuna majengo upande mmoja (Magharibi) mwa soko hilo majengo yake yanayotumika kama maduka madogo ni ya kiwango kidogo huku yakiwa yamechakaa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inatambua kuwa soko jipya la Kwa Mrombo linalojengwa ni la kisasa. Kamati inaona kuwa upande wenye majengo ya hali ya chini na yaliyochakaa hayataleta sura nzuri kwa soko la kisasa linalojengwa. Kamati inatambua kuwa maeneo hayo pamoja na majengo yake ni mali ya Halmashauri ya Jiji la Arusha.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

Serikali ihakikishe wananchi waliokuwa wanafanya biashara zao katika soko hili wanapewa kipaumbele cha kupewa nafasi kuendelea na biashara zao;

### 2.1.13 Ujenzi wa Soko la Kilombero

**Mheshimiwa Spika;** Mradi wa Ujenzi wa Soko la Kilombero unatekelezwa katika eneo lenye mita za mraba 18,215, ambapo jumla ya eneo litakalojengwa ni mita za mraba 10,885, ikihusisha uboreshaji wa mazingira ya nje *(landscaping),* mifumo ya maji ya mvua, maji taka pamoja na miundombinu ya kisasa ya Maegesho ya magari na vyombo vingine vya moto.

***Mheshimiwa Spika***; utekelezwaji wa mradi huu unaogharimu Shilingi 9,502,042,553, unatekelezwa na Kampuni ya **M/S MOHAMMED BUILDERS LIMITED** na unasimamiwa na Mhandisi Mshauri kutoka kampuni ya **Mhandisi Consultancy Ltd** kwa ushirikiano na kampuni ya **GBS Consultant** Ltd za Dar es Salaam.

**Hatua za Utekeleza wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** hadi kufikia wakati wa ukaguzi wa mradi huu mkandarasi tayari alikuwa ameshalipwa asilimia 41.66%, ambayo ni shilingi 3,958,851,898,00.

***Mheshimiwa Spika***; Soko hili limesanifiwa kuwa na miumbombinu mbalimbali ikiwemo, Vizimba 518, vitakavyopokea wafanyabiashara 2,072 kwa wakati mmoja; maliwato ya kike na ya kiume, vyumba viwili vya mapumziko kwa kina mama wajawazito na wanaonyonyesha watoto vyenye uwezo wa kuweka vitanda 32 kwa wakati mmoja, vyumba viliwi vya Ibada kwa dini za Kikristu na dini ya Kiisalamu, maeneo manne (4) kwa maduka makubwa, benki, ofisi na huduma nyinginezo, vyumba viwili vya kuhifadhia mazao yanayoweza kuharibika kama vile nyama na vinginevyo *(cold rooms),* kituo cha polisi, chumba cha huduma ya kwanza, miundombinu rafiki inayokidhi mahitaji ya watu wote kufikia sehemu zote za soko ikiwemo ngazi ya watu wenye ulemavu *(ramp)* na ngazi pande zote mbili; eneo la bustan kwa ajili ya mapuziko ya Wafanyabiashara na Wateja na maegesho ya vyombo vya moto.

**Changamoto**

***Mheshimiwa Spika***; utekelezaji wa Mradi huu umekumbwa na changamoto ya upatikanaji wa vifaa vya ujenzi, hali iliyochelewesha mkandarasi kuweza kufikia lengo kwa asilimia 5%, ambapo sasa mradi huu umeongezewa muda wa miezi sita ili kukamilika, badala ya tarehe 30/05/2026.

**Uchambuzi wa Kamati**

**a) Uchakavu wa Soko la Awali la Kilombero**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Soko Kuu la Kilombero Mkoani Arusha linajengwa pembeni kidogo ya Soko Kuu la Zamani la Kilombero. Kamati imebaini kuwa soko hilo la zamani ni soko duni, na kwamba ni soko lililochakaa kwa kiwango kikubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa katika usanifu wa soko jipya limewekwa daraja litakalounganisha soko jipya na soko la zamani. Kamati inapongeza sana ubunifu huo. Hata hivyo, Kamati inaona kuwa Soko Kuu la Kilombero la zamani lina hali mbayá sana kwa miundombinu yake. Kamati inaona kuwa kuunganisha daraja kati ya Soko Kuu Jipya la Kilombero lenye miundombinu ya kisasa na lenye ubora wa hali ya juu ni kutolitendea haki Soko hili.

**b) Usanifu wa Soko unaokidhi matumizi ya kisasa ya Masoko ya Kimataifa**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Soko Kuu la Kilombero la Mkoa wa Arusha limesanifiwa kwa usanifu wa kisasa unaokidhi mahitaji yote muhimu ya binadamu yanayohusiana na masoko. Kamati imeona kuwa soko hili lina maeneo maalum kwa ajili ya akina mama walio na watoto ambalo litatumika kwa ajili ya kuwanyonyesha watoto. Aidha, soko lina sehemu maalum iliyowekwa kwa ajili ya watu wa dini ya Kiislam na Kikristu kufanya ibada kwa nyakati tofautitofauti. Usanifu wa soko umetenga hata maeneo kwa ajili ya taasisi za fedha kama vile benki na kadhalika. Kamati inaipongeza sana Serikali kwa usanifu huu maridadi.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

(a) Serikali ihakikishe utekelezaji wa ujenzi wa mradi unakamilika ndani ya muda uliokusudiwa;

(b) Serikali ihakikishe wananchi waliokuwa wanafanya biashara zao katika soko hili wanapewa kipaumbele cha kupewa nafasi kuendelea na biashara zao;

### 2.1.14 Mradi wa Uboreshaji wa Bustani ya Mapumziko Themi (*Themi living Garden*)

***Mheshimiwa Spika***; Mradi wa Uboreshaji wa Bustani ya Mapumziko Themi unatekelezwa na Kampuni ya M/S MOHAMMED BUILDERS LIMITED kwa gharama ya shilingi 1,315,655,048.00, na unasimamiwa na mhandisi mshauri kutoka kampuni ya Mhandisi Consultancy Ltd kwa ushirikiano na kampuni ya GBS Consultant Ltd za Dar es Salaam.

**Faida za Mradi**

***Mheshimiwa Spika***; faida zitakazopatikana kutokana na mradi huu ni pamoja na kuongeza ajira, kipato cha wananchi, pamoja na mapato ya Halmashauri ya Jiji la Arusha.

**Chagamoto za Utekelezaji Mradi**

***Mheshimiwa Spika***, utekelezaji wa mradi huu ambao mpaka kufikia tarehe ya ukaguzi wa mradi ulikuwa umefikia asilimia 20.17% ya utekelezaji wake, ulipangwa kuanza tarehe 30/05/2025 na kukamilika tarehe 30/05/2026, ulikumbwa na changamoto mbalimbali zikiwemo michoro ya usanifu iliyokuwa imeandaliwa awali haikuwa ya kina kwa baadhi ya maeneo kutokana na asili ya eneo la bustani pamoja na uwepo wa mimea adimu, na ukamilishaji wa mapitio ya usanifu (design review) kwa kina hali iliyopelekea utekelezaji wa mradi kuchelewa kuanza na badala yake kuanza tarehe 09/10/2025.

**Uchambuzi wa Kamati**

**Usanifu wa Mradi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa usanifu wa mradi huu ni wa kisasa na unaoweza kuhudumia (to accommodate) watu wa aina zote. Bustani ina maeneo kwa ajili ya watu kuembea kwa miguu, kuna maeneo kwa ajili ya kutembea bila kuvaa viatu, maeneo kwa ajili ya viburudisho na vinywaji, madaraja na mambo mengi yanayofanana na hayo. Kamati inapongeza usanifu wa bustani hii.

**Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inashauri Serikali ihakikishe kuwa mradi wa uboreshaji wa Bustani ya Mapumziko Themi unakamilika kwa wakati ili wananchi waweze kufaidika na huduma iliyokusudiwa;

## 2.2 Tathmini ya Jumla ya Utekelezaji wa miradi, kwa miradi iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2025/2026, kutembelewa na kukaguliwa na Kamati

**Mheshimiwa Spika,** baada ya Kamati kufanya ukaguzi wake wa miradi katika mikoa ya Morogoro, Pwani, Kilimanjaro na Arusha imefanya uchambuzi wa jumla wa ukaguzi wake kama ifuatavyo: -

### 2.2.1 Udhaifu wa Utekelezaji wa Miradi katika Mkoa wa Morogoro

**Mheshimiwa Spika,** Katika ukaguzi wake Kamati imebaini kuwa kumekuwa na udhaifu wa utekelezaji wa miradi katika Mkoa wa Morogoro. Miradi kama ujenzi wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro pamoja na ujenzi wa Stendi ya mabasi madogo ya Mji wa Mikumi. Aidha, utekelezaji wa miradi ya Barabara ya Muhimbili na Stendi ya Magari Madogo ya Kihonda katika mkoa huo ni ya kuridhisha.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati pia imebaini kuwa ujenzi wa miradi ya shule katika Mkoa wa Arusha imekuwa na kasoro kadha wa kadha kama vile ukosefu wa maji katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Longido Samia, ukosefu wa uzio katika shule ya Wasichana ya Longido Samia, Shule ya Awali na Msingi ya Lowasa pamoja na Shule ya Sekondari ya Migungani One.

**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla, baada ya Kamati kufanya ukaguzi wa miradi katika miradi yote, Kamati imebaini kuwa utekelezaji wa miradi umewezeshwa kwa kutumia fedha za ndani. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii. Hii ni dalili njema ya Serikali yetu kuanza kujitegemea katika kutekeleza mambo yake ya msingi,

hasa miradi ambayo ina kipaumbele cha juu kwa wananchi wa Tanzania.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati imebaini kuwa miradi inayotekelezwa na Halmashauri nchini ina changamoto nyingi kuliko inayotekelezwa na taasisi zilizo chini ya OWM-TAMISEMI. Kamati inadhani kuwa kunaweza kukawa na changamoto ya usimamizi wakati wa utekelezaji wa miradi hiyo kwa ngazi ya Halmashauri. **Kamati inashauri OWM-TAMISEMI kuimarisha usimamizi katika utekelezaji wa miradi ya Halmashauri nchini**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa katika miradi mingi inayosimamiwa na Halmashauri iliyotembelewa na kukaguliwa kumekuwa na changamoto ya usanifu. Kwa mfano, mradi wa Hospitali ya Halmashauri ya Manispaa ya Morogoro umesanifiwa kujengwa katika eneo ambalo ni oevu. Aidha, ujenzi wa stendi ya Mabasi ya Mikumi umepangwa kujengwa katika eneo oevu lakini pia lililo eneo ambalo si rafiki kwa matumizi ya stendi. Vilevile, Soko Kuu la Mkoa wa Arusha limesanifiwa bila kuzingatia soko la zamani huku soko hilo la zamani likitegemewa kuendelea kutumika. Stendi Kuu ya Mabasi ya Mkoa wa Arusha ilisanifiwa kujengwa katika eneo ambalo lina njia kubwa ya umeme. **Kwa hali hiyo, Kamati inashauri kuwa miradi yote inayosanifiwa kutekelezwa na halmashauri, kabla ya kuomba bajeti Wizara ya TAMISEMI itume timu ya kufanya ukaguzi na kujiridhisha kuhusu usanifu na upembuzi yakinifu uliofanyika kwa ajili ya miradi hiyo. Kamati inaendelea kushauri kuwa, Serikali izingatie kanuni za uendeshaji miradi (*Principles of Projects Management*) kwa kufanya upembuzi yakinifu *(Feasibility study)* na Tathmini ya Athari kwa Mazingira (*Enviromental Impact Assessment*) kabla ya kuanza utekelezaji wa miradi ili kuhakikisha miradi inayotekelezwa inaleta athari chanya na tija iliyokusudiwa kwa jamii;**

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAONI YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2025/2026

**Mheshimiwa Spika**, Baada ya Wizara pamoja na Sekretarieti za Mikoa kuwasilisha Bajeti zao kwa mafungu 28 Kuanzia tarehe 19 hadi tarehe 30 Machi, 2026, Kamati ilipata wasaa wa kuichambua na kuijadili, lakini pia Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo mbalimbali kwa lengo la kuboresha utendaji kazi wa Wizara kama ifuatavyo:-

### 3.1 Utekelezaji wa Maoni, Ushauri na Mapendekezo ya Kamati kwa Mwaka 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** katika taarifa ya Kamati iliyowasilishwa Bungeni kuhusu bajeti ya Wizara kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, Kamati ilitoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo nane (8). Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, kwa kiasi kikubwa Serikali imetekeleza Maoni na Ushauri wa Kamati. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanyia kazi Maoni na Ushauri huo.** Aidha, kwa maeneo ambayo bado hayajatekelezwa kikamilifu Kamati itaendelea kuyasisitiza katika taarifa hii likiwemo, suala la shule za mchepuo wa Kiingereza, upungufu/uhaba wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini, na madeni ya watumishi katika Halmashauri nchini.

## 3.2 Uchambuzi wa ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

**Mheshimiwa Spika,** Wizara kupitia **Fungu 56** (Makao Makuu ya Wizara), Fungu 02 (Tume ya Utumishi wa Walimu) na Mafungu 26 kutoka Sekretarieti za Mikoa katika Mwaka wa Fedha 2025/2026 ilikadiria kukusanya maduhuli ya **Shilingi 1,925,881,323,464.00.** Kati ya fedha hizo, **Shilingi 188,960,306,000.00** sawa na **asilimia 9.8** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 1,644,835,000.00** sawa na **asilimia 0.09** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Shirika la Elimu Kibaha; **Shilingi 21,721,743,786** sawa na **asilimia 1.2** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka – Dar es Salaam (DART); **Shilingi 10,745,182,213.00** sawa na **asilimia 0.6** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa; **Shilingi 3,506,815,065** sawa na **asilimia 0.25** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa; **Shilingi 7,000,000,000.00** sawa na **asilimia 0.36** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA); **Shilingi 11,489,598,000.00** sawa na **asilimia 0.59** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo; **Shilingi 306,108,174,064.00** sawa na **asilimia 0.015** zilikadiriwa kukusanywa kutoka Ofisi za Mikoa na **Shilingi 1,680,506,764,000** sawa na **asilimia 87.2** zilikadiriwa kukusanywa kutoka katika Halmashauri. *(Kwa maelezo zaidi tazama Jedwali Namba 1.*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitaarifiwa kwamba, hadi Mwezi Februari 2026, jumla ya **Shilingi 1,161,087,740,803.41** zilikusanywa, sawa na **asilimia 90.43** ya lengo la makusanyo yote kwa mwaka. Kati ya fedha hizo **Shilingi 61,133,297,699.50** sawa na **asilimia 5.26**

zilikusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, **Shilingi 954,965,067.69** sawa na **asilimia 0.08** kutoka Shirika la Elimu Kibaha; **Shilingi 3,736,392,132** sawa na **asilmia 0.32** kutoka Wakala wa Mabasi yaendayo Kasi Dar es Salaam (DART), **Shilingi 5,316,295,239.00** sawa na **asilimia 0.45** kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, **Shilingi 757,866,828.21** sawa na **asilimia 0.0065** kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, **Shilingi 2,324,910,186.15** sawa na **asilimia 0.2** kutoka Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA); **Shilingi 839,795,987.56** sawa na **asilimia 0.07** kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo, **Shilingi 172,874,155.3** sawa na **asilimia 0.014** kutoka Makao Makuu ya Mikoa na **Shilingi 1,085,852,343,508.00** sawa na **asilimia 93.5** kutoka halmashauri. *(Tazama Kielelezo Na. 1)*


JEDWALI NA 1: *Hali ya ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka 2025/2026, hadi mwezi Februari, 2026*

| Taasisi | Makisio | Kiasi Kilichokusanywa | Asilimia ya makusanyo |
|---|---|---|---|
| Makao Makuu ya Wizara | 188.960,306,000 | 61,133,297,699.50 | 48.53 |
| Shirika la Elimu Kibaha | 1,644,835,000.00 | 954,965,067.69 | 87 |
| Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam (DART) | 21,721,743,786.00 | 3,736,392,132.00 | 25.80 |
| Chuo cha Serikali za Mitaa | 10,745,182,213.00 | 5,316,295,239.00 | 7.21 |
| Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa | 3,506,815,065.00 | 756,866,828.21 | 32.37 |
| Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) | 7,000,000,000 | 2,324,910,186.15 | 49.82 |

| | | | |
|---|---|---|---|
| Shirika la Masoko ya Kariakoo | 11,489,598,000.00 | 839,795,987.56 | 10.96 |
| Maduhuli - Mikoa | 306,079,400.00 | 172,874,155.30 | 84.72 |
| Halmashauri za Wilaya | 1,680,506,764,000 | 1,085,852,343,508 | 96.92 |

***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

KIELELEZO NA 1: *Mwenendo wa Makusanyo ya Maduhuli ya OR-TAMISEMI (Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu 26 ya mikoa kwa mwaka 2025/2026*




***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*


**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa kati ya taasisi zote zilizo chini ya OWM-TAMISEMI Halmashauri za Wilaya ndizo zilizofanya vyema kwenye makusanyo ya maduhuli ambapo zimekusanya maduhuli kwa **asilimia 90** ya makadirio yake. Kiasi hiki ni kikubwa ukilinganisha na asilimia 66 iliyotarajiwa kufikiwa hadi mwezi Februari, 2026. Kamati ilihoji sababu ya makusanyo hayo kuwa makubwa kwa kiwango hicho na kujibiwa kuwa ni kutokana na matumizi ya mifumo mbalimbali ya ukusanyaji wa mapato iliyoanzishwa na Wizara kwa Halmashauri. Kamati inapongeza hatua hii. Kamati inashauri Wizara iendelee kuimarisha ukusanyaji wa mapato katika halmashauri na taasisi zake zote.

**Mheshimiwa Spika,** aidha, Kamati imebaini kuwa Shirika la Masoko ya Kariakoo ndilo lililo chini zaidi katika makusanyo ya maduhuli. Hadi mwezi Februari, 2026 Shirika hilo lilikuwa limekusanya maduhuli kwa asilimia 10.9 badala ya asilimia 66 iliyotarajiwa hadi mwezi Februari, 2026. Kamati ilihoji ili kufahamu sababu ya Shirika la Masoko ya Kariakoo kukusanya kiwango cha chini zaidi na kujulishwa kwamba ni kutokana na soko hilo kuzinduliwa Mwezi Februari, 2026.

**Mheshimiwa Spika,** matarajio ya Kamati ilikuwa OWM-TAMISEMI, taasisi zake pamoja Sekretarieti za Mikoa, kufikia asilimia 66 ya makusanyo ya maduhuli hadi Februari, 2026. Hata hivyo, taasisi zilizokusanya maduhuli yake kuzidi asilimia 66 iliyowekwa ni nne tu kati ya tisa. Kamati imebaini kuwa makusanyo ya OWM-TAMISEMI yameonekana kuwa juu kwa sababu ya taasisi mbili zilizo chini ya Wizara za Shirika la Elimu Kibaha (asilimia 87.09) na Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo) (asilimia 74.21). Aidha, Makao Makuu ya Mikoa pamoja na Halmashauri zimekusanya

maduhuli, hadi mwezi Februari, 2026 kwa asilimia 74.21 na 96.92 mtawalia.

KIELELEZO NA 2: *Makadirio ya makusanyo ya maduhuli na asilimia ya makusanyo halisi kwa mwaka 2024/2025*




***Chanzo***: *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

**Ulinganisho wa Makusanyo ya Maduhuli kuanzia mwaka 2023/2024 – 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika**, Kamati imebaini kuwa kumekuwa na mwendelezo mzuri wa upangaji wa makisio katika OWM-TAMISEMI, taasisi zake pamoja na Makao Makuu ya Mikoa na Halmashauri zake kwa muda wa miaka mitatu mfululizo. Hali hii inaonesha kuwa vyanzo vya mapato kwenye OWM-TAMISEMI vinaendelea kukua na kuimarika kila mwaka. Kamati inaamini kuwa hali hii inatokana na kukua kwa uchumi kwenye Mamlaka za Serikali za Mitaa, kuimarisha usimamizi wa mapato pamoja na kubuni njia nzuri za ukusanyaji wa mapato na kuendelea kuzuia mianya ya upotevu wa mapato; na hivyo kuchagiza ustawi wa jamii. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuweka mikakati inayosababisha ukuaji huu wa uchumi na maendeleo kwa jamii.**


**JEDWALI NA 2:** *Makusanyo ya Maduhuli kwa ulinganisho kuanzia Mwaka wa Fedha 2023/2024 – 2025/2026 kwa miaka mitatu mfululizo*

| NA. | Taasisi | 2023/2024 | 2024/2025 | 2025/2026 |
|---|---|---|---|---|
| | Makao Makuu ya Wizara | 0 | 188,960,306,000 | 188,960,306,000 |
| | Shirika la Elimu Kibaha | 1,634,835,000.00 | 1,634,835,000 | 1,644,835,000 |
| | Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam (DART) | 17,172,749,540.00 | 21,577,652,305 | 21,721,745,786 |
| | Chuo cha Serikali za Mitaa | 10,437,966,865.00 | 10,535,182,220 | 10,745,182,213 |
| | Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa | 4,131,215,065.00 | 4,131,215,065 | 3,506,815,065 |
| | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) | 15,200,000,000.00 | 5,600,000,000 | 7,000,000,000 |
| | Shirika la Masoko ya Kariakoo | 6,565,654,276.00 | 11,948,802,000 | 11,489,598,000 |
| | Maduhuli - Mikoa | 261,890,400.00 | 315,939,400 | 306,079,400 |
| | Halmashauri | 1,143,883,281,000 | 1,356,340,664,000 | 1,680,506,764,000 |
| | **JUMLA** | **1,199,287,592,146** | **1,601,044,595,990** | **1,925,881,323,464** |


***Chanzo***: *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake pia Kamati ilibaini kuwa kuna ongezeko la utengaji wa makisio ya makusanyo ya maduhuli kutoka **Shilingi 1,199,287,592,146** zilizotengwa mwaka 2023/2024 hadi **Shilingi 1,925,881,323,464** zilizotengwa kwa mwaka **2025/2026,** sawa na ongezeko la **Shilingi 726,593,731,318** sawa na **asilimia 60.5**. Kamati inaipongeza Serikali kwa hatua hii. Kamati inaamini kuwa mapato hayo yataendelea kuongezeka kutokana na kukua kwa uchumi, kuongezeka kwa idadi ya watu na kuongezeka kwa shughuli za wananchi nchini. Kamati inashauri Serikali iendelee kubuni vyanzo vya kuimarisha mapato ili kuendelea kukuza uchumi na hivyo kuleta ustawi kwa wananchi.

**Kielelezo Na. 3:** *Mwenendo wa Utengaji wa Makisio ya Maduhuli kuanzia 2023/2024 hadi 2025/2026 kwa bilioni*




Kielelezo Na. 4: *Mwenendo wa Utengaji wa Mapato na Matumizi ya OWM-TAMISEMI kwa mud awa miaka mitatu  mfululizo 2023/2024 hadi 2025/2026*




***Chanzo**: Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na ya taarifa ya Wizara kwa ulinganisho wa randama za vipindi vitatu tofauti Kamati imebaini kuwa Halmashauri zimeendelea kufanya vyema kwenye utengaji na ukusanyaji wa maduhuli ambapo unaongezeka kila mwaka wa Fedha. Wakati huo huo, Kamati imebaini kuwa Makao Makuu ya Wizara pamebaki na makadirio yaleyale ya makusanyo ya maduhuli kwa miaka miwili mfululizo. Aidha, makadirio ya ukusanyaji wa maduhuli katika Makao Makuu ya Mikoa yamekuwa yakishuka kwa miaka miwili mfululizo. **Kamati inashauri Makao Makuu ya Wizara pamoja na Makao Makuu ya Mikoa kubadilisha mtazamo huo na kuanza kubuni vyanzo vipya vya mapato.**

**Mheshimiwa Spika,** kwa upande wa ukusanyaji wa maduhuli hadi mwezi Februari ya kila mwaka kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizo, kuanzia mwaka 2023/2024 hadi mwaka 2025/2026 kumekuwa na ongezeko katika Halmashauri. Kamati inazipongeza sana Halmashauri kwa juhudi zake. Hii inaonesha kuwa halmashauri zimeendelea kuwa bunifu katika kuongeza vyanzo vya mapato, na hivyo kuendelea kujenga uwezo wa halmashauri katika kuhudumia wananchi.

**Mheshimiwa Spika,** Katika uchambuzi wake pia Kamati imebaini kuwa kwa ujumla mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa taarifa zinazoishia mwezi Februari kwa kila mwaka Wizara, taasisi zake na Mikoa 26 imekuwa ikiongezeka. Mwenendo wa ukusanyaji wa mapato kwa ujumla umekuwa ukikua kutoka **shilingi 756,389,752,472.27 mwaka 2023/2024 hadi shilingi 1,161,087,740,803.41 mwaka 2025/2026. Hili ni ongezeko la shilingi 404,697,988,331.14,** sawa na asilimia 53.5. Kamati inasifu mwenendo huu wa ukusanyaji wa maduhuli.

**Mheshimiwa Spika,** hata hivyo, Kamati pia imebaini pamoja na ukuaji huo wa ukusanyaji wa maduhuli kwa kipindi hicho kukua bado kuna taasisi ambazo mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli umekuwa ukishuka. Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam (DART) makusanyo yake yamekuwa yakishuka kwa kipindi cha miaka ya fedha 2024/2025 na 2025/2026 kwa shilingi 4,969,343,555.00 na shilingi 3,736,392,132.00 mtawalia. Aidha, Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo) mapato yake yamekuwa yakishuka katika kipindi cha Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026 kwa shilingi 5,063,370,896.00 na shilingi 3,316,295,239.00 mtawalia.


Jedwali Na. 3: *Ulinganisho wa mwenendo wa makusanyo ya maduhuli kuanzia mwaka 2023/2024 hadi 2025/2026*

| NA. | Taasisi | 2023/2024 | 2024/2025 | 2025/2026 |
|---|---|---|---|---|
| 1 | Makao Makuu ya Wizara | 0 | 48,957,910,165.36 | 61,133,297,699.50 |
| 2 | Shirika la Elimu Kibaha | 784,156,491.50 | 810,710,840.00 | 954,965,069.69 |
| 3 | Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar-es-Salaam (DART) | 5,859,457,872.73 | 4,969,343,555.00 | 3,736,392,132.00 |
| 4 | Chuo cha Serikali za Mitaa | 4,881,583,363.61 | 5,063,370,896.00 | 3,316,295,239.00 |
| 5 | Bodi ya Mikopo ya | 437,544,255.44 | 598,232,080.07 | 756,866,828.21 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | Serikali za Mitaa | | | |
| 6 | Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) | 1,555,811,906.48 | 1,002,864,956.17 | 2,324,910,186.15 |
| 7 | Shirika la Masoko ya Kariakoo | 190,185,134.51 | 129,837,745.77 | 839,795,987.56 |
| 8 | Maduhuli - Mikoa | 193,798,600.00 | 130,925,932.00 | 172,874,155.30 |
| 9 | Halmashauri | 742,487,214,848 | 818,236,439,347.78 | 1,085,852,343,508.00 |
| **JUMLA** | | **756,389,752,472.27** | **879,899,635,518.15** | **1,161,087,740,803.41** |

**Chanzo**: *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

**Kielelezo Na. 5:** *Mwenendo wa ukusanyaji wa maduhuli hadi mwezi Februari, kwa kipindi cha miaka mitatu mfululizi (2023/2024 – 2025/2026 (OWM – TAMISEMI)*




**Chanzo**: *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2025)*

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na kielelezo cha hapo juu sura ya ukusanyaji wa maduhuli kwa upande wa Halmashauri hadi mwezi Februari ya kila Mwaka wa Fedha husika (2023/2024 – 2025/2026) umekuwa ukiongezeka.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa Halmashauri zimefanikiwa kuongeza makusanyo ya maduhuli kutoka shilingi **756,389,752,472.27 h**adi **shilingi 818,236,439,347.78,** kwa Mwaka wa Fedha 2023/2024 na 2024/2025, ambapo ni ongezeko la **shilingi 61,846,686,875.51**, sawa na **asilimia 8.2 kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 na 2025/2026** makusanyo ya maduhuli yamepanda kutoka **shilingi 818,236,439,347.78** hadi shilingi **1,085,852,343,508.00,** sawa na ongezeko la **shilingi 267,615,904,161,** sawa **na asilimia 32.7**. **Kamati inapongeza sana juhudi za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa makusanyo hayo.**


**Utolewaji fedha za matumizi kwa Mwaka 2025/2026**

**Mheshimiwa Spika,** katika Bajeti ya mwaka 2025/2026 iliyopitishwa na Bunge lako Tukufu Juni, 2024 Wizara kupitia Fungu 56, Fungu 02 pamoja na mafungu 26 ya mikoa iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 11,612,594,336,000.** Kati ya fedha hizo **Shilingi 7,836,140,708,000.00** sawa na **asilimia 67.5** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 3,776,453,628,000.00** sawa na **asilimia 32.5** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya fedha za matumizi ya kawaida ambazo ni **Shilingi 7,836,140,708,000.00, Shilingi 6,292,557,648,000.00** sawa na **asilimia 80.3** ni kwa ajili ya mishahara na **Shilingi 1,543,583,060,000.00** sawa na **asilimia 19.7** ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

**Mheshimiwa Spika,** hadi Mwezi Februari, 2026 Wizara, taasisi zake pamoja na Sekretarieti za Mikoa zilipokea jumla ya Shilingi **7,293,003,173,591.86** sawa na **asilimia 62.8** ya fedha zilizoidhinishwa. Kati ya fedha hizo, Shilingi **5,501,410,966,448.14** sawa na **asilimia 75.4** ni kwa ajili ya matumizi ya kawaida na **Shilingi 1,791,592,207,143.72** sawa na **asilimia 24.6** ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo. Kati ya **Shilingi 5,501,410,966,448.14** za matumizi ya kawaida zilizopokelewa **Shilingi 4,299,038,507,722.81** sawa na **asilimia 78.1** ni kwa ajili ya matumizi ya mishahara na **shilingi 1,202,372,458,725.33** sawa na **asilimia 17.9** ni kwa ajili ya matumizi

mengineyo *(OC)*. Aidha, kati ya Shilingi **1,791,592,207,143.72** za matumizi ya maendeleo zilizopokewa **Shilingi 1,597,047,240,601.97** sawa na **asilimia 89.1** ni fedha za ndani na shilingi **194,544,966,541.75** Sawa na **asilimia 10.9** ni fedha za nje. *(Tazama Jedwali Na. 4 pamoja na Kielelezo 6)*

Kielelezo Na 6. *Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa hadi Februari, 2026 (OWM-TAMISEMI)*





**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi kuhusu mwenendo huu wa upokeaji wa fedha na kubaini mambo kadhaa kama ifuatavyo: -

**a) Mwenendo wa upokeaji wa fedha za matumizi ya kawaida na za maendeleo**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kuwa fedha kwa ajili ya miradi miradi ya maendeleo zilizopokelewa ni asilimia 24.6 tu. Aidha, fedha za maendeleo kutoka vyanzo vya ndani zilizopokelewa ni asilimia 89.1 ya fedha zote za maendeleo zilizopokelewa, wakati huohuo fedha za maendeleo zilizopokelewa kutoka vyanzo vya nje ni asilimia 10.9 tu. **Kamati inaipongeza Serikali kwa kuhakikisha fedha za miradi kutoka vyanzo vya ndani inapelekwa kwa kiwango cha juu.**

**Mheshimiwa Spika,** mwenendo huu wa upokeaji wa fedha za maendeleo kutoka nje unakwamisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri na mikoa yetu nchini utaathirika. Hii ni dalili kuwa ukuaji wa maendeleo jumuishi kwa wananchi unaanza kurudi nyuma. Hali hii inarudisha nyuma juhudi za Serikali za kukuza uchumi na ustawi wa wananchi. **Kamati inashauri kuwa Serikali iweke mikakati mahsusi na kabambe ya kuhakikisha kwamba inaanza kutenga bajeti yake kwa ajili ya miradi ya maendeleo kwa kutegemea zaidi vyanzo vyake vya ndani kuliko kutegemea vyanzo vya nje. Kamati inaendelea kushauri Halmashauri ziendelee kuongeza mikakati ya kuibua vyanzo vipya vya mapato na kuendelea kuimarisha ukusanyaji wa mapato**.

Kielelezo Na 7. *Ulinganisho wa fedha zilizoidhinishwa na zilizopokelewa hadi Februari, 2026*





***Chanzo***: *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

**Jedwali Na 4.** *Mchanganuo wa mapokezi ya fedha hadi Februari, 2026*

| MATUMIZI YA KAWAIDA | | MATUMIZI YA MAENDELEO | |
|---|---|---|---|
| **Mishahara** | **Mengineyo** | **Ndani** | **Nje** |
| 4,299,038,507,722.81 | 1,202,372,458,725.33 | 1,597,047,240,601.97 | 194,544,966,541.75 |
| **5,501,410,966,448.14** | | **1,791,592,207,143.72** | |

***Chanzo***: *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

***Kielelezo Na 8.*** *Upokeaji wa fedha za matumizi ya kawaida na miradi ya maendeleo OWM-TAMISEMI hadi Februari, 2026*




***Chanzo***: *Randama ya Wizara na Usanifu wa Kamati (Aprili 1, 2026)*

## SEHEMU NNE

## 4.0 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imetaarifiwa kuwa Bajeti ya mwaka 2026/27 ya OWM Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa itatekeleza vipaumbele katika usimamizi wa utawala bora; ukusanyaji wa mapato ikijumuisha mapato yanayotokana na hewa ukaa, ujenzi wa miundombinu kwenye sekta za barabara, elimu na afya, kusimamia mifumo ya TEHAMA, uendelezaji wa vijiji na miji, na kujenga uwezo wa watumishi katika ngazi zote za usimamizi wa Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI. Kamati imeridhishwa na vipaumbele hivyo vilivyowekwa na Wizara.


**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa mchanganuo wa shughuli zilizopangwa kutekelezwa na Wizara kwa kuzingatia vipaumbele vilivyowekwa na Wizara kwa mwaka wa fedha 2025/2026 kama ifuatavyo: -

### 4.1 Uchambuzi wa Makadirio ya Ukusanyaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 Wizara pamoja na taasisi zake, (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu 02) pamoja na Mamlaka za Serikali za Mitaa (Mafungu 26) imekadiria kukusanya maduhuli ya jumla ya **shilingi 2,336,528,152,302.47.** Hili ni ongezeko la **shilingi 412,291,663,838.47** kutoka **shilingi 1,924,236,488,464.00** iliyokadiriwa kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026, sawa na asilimia 21.4**.** *(Tazama kielelezo Na 9)* Kati ya fedha hizo **Shilingi 188,960,306,000.00,** shilingi zimekadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Wizara, shilingi 22,922,343,786.00 kutoka Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART), shilingi 125,115,565,696.00 kutoka Kampuni ya Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (UDART), shilingi


11,922,250,620.20 kutoka Chuo cha Serikali za Mitaa, shilingi 4,220,034,839.27 kutoka Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa, shilingi 5,400,000,000.00 kutoka kwa Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA), na **shilingi 11,489,598,000.00** kutoka Shirika la Masoko ya Kariakoo. Aidha, shilingi 305,050,361.00 zinakadiriwa kukusanywa kutoka Makao Makuu ya Mikoa, na s**hilingi 1,966,193,000,000.00** zimekadiriwa kukusanywa kutoka Halmashauri.

Kielelezo Na. 9: **Ulinganifu wa Utengaji wa Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 na 2026/2027**




**Mheshimiwa Spika,** kwa ujumla makisio ya ukusanyaji wa maduhuli yameongezekaka kwa Halmashauri za Wilaya, Bodi ya Mikopo ya Serikail za Mitaa, Chuo cha Serikali za Mitaa (Hombolo), pamoja na Wakala wa Mabasi Yaendayo Haraka Dar es Salaam (DART) (Tazama kielelezo Na 10) . **Kamati inapongeza Halmashauri pamoja na taasisi za TAMISEMI zilizoongeza makisio ya ukusanyaji wa maduhuli**.

**Kielelezo Na 10. Makadirio ya Maduhuli kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027**




**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na kielelezo hapo juu Kamati imebaini kuwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa imeongoza kwa kupanga kukusanya maduhuli kwa asilimia 30 ikifuatiwa na Halmashauri. Kamati imetaarifiwa kuwa ongezeko la makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa limetokana na Halmashauri nne, (4) za Songea MC, Makambako TC, Kasulu TC na Nyangh'wale DC ambazo zimekopeshwa na Bodi, na kwamba, zitaanza kurejesha mikopo yao mwaka 2026/27; Kuwekwa Kifungu Maalum cha kutenga marejesho ya mikopo na MCR kwenye mfumo wa PlanRep kudhibiti utengaji na uidhinishwaji wa fedha hizo kuhakikisha kuwa zinawasilishwa bodi kama zilivyokasimiwa. Aidha, kwa upande wa Halmashauri Kamati imeelezwa kuwa kufanyika kwa tathmini ya makusanyo ya mapato ya ndani kwa ajili ya uandaaji wa Mipango na Bajeti katika mwaka wa fedha 2025/26 na hivyo kuongeza makisio ya mapato ya ndani kumefanya makisio

ya makusanyo ya maduhuli kuongezeka. Aidha, matumizi sahihi ya Mfumo wa kukusanyia Mapato wa TAUSI umedhibiti makusanyo yote ambayo yalikuwa yanakusanywa nje ya bajeti na hivyo kulazimisha Halmashauri kuiingiza katika bajeti za makusanyo.

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (TARURA) imepunguza makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa asilimia 22 huku Sekretarieti za Mikoa zikipunguza makisio ya makusanyo yake ya maduhuli kwa asilimia 0.34. Kamati imetaarifiwa kuwa TARURA imepunguza ukomo wa mapato ya ndani kutokana na mabadiliko na kushuka kwa ada ya utozaji ya matumizi ya hifadhi ya barabara kulikosababishwa na mabadiliko ya sheria kwenye viwango vya utozaji wa ada hizo. Aidha, Makadirio ya makusanyo ya maduhuli katika ofisi za wakuu wa mikoa yamepungua kutokana na baadhi ya kumbi za mikutano kutumika kwa ajili ya vikao vya ndani vya serikali na kufanyika kwa ukarabati wa kumbi za mikutano na migahawa.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wake, Kamati pia imebaini kuwa Makao Makuu ya Wizara pamoja na Shirika la Masoko ya Kariakoo makadirio yao ya maduhuli hayakuongezeka wala kupungua. Kamati ilihoji sababu ya makisio hayo kutokuongezeka wala kupungua na kutaarifiwa kuwa; kwa upande wa Makao Makuu ya Wizara sababu iliyoelezwa ni kutokana na jukumu la ukusanyaji wa kodi ya majengo kupewa Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, kwa upande wa Shirika la Masoko ya Kariakoo, Kamati ilitaarifiwa kwamba ni kutokana na Shirika kutenga bajeti kama hiyo mwaka wa 2025/2026 kwa matarajio ya soko

kufunguliwa rasmi lakini halikufunguliwa kutokana na sababu mbalimbali, hivyo kulilazimu shirika kurejea makadirio yale yale.


Jedwali Namba. 5: *Mwenendo wa utengaji wa makisio ya makusanyo ya maduhuli kwa kipindi cha 2024/2025 hadi 2026/2027*


| TAASISI | KIWANGO CHA MADUHULI KILICHOPANGWA | | |
|---|---|---|---|
| | 2024/2025 | 2025/2026 | 2026/2027 |
| OWM-TAMISEMI | 188,960,306,000 | 188,960,306,000 | 188,960,306,000 |
| Shirika la Elimu Kibaha | 1,634,835,000.00 | 1,644,835,000 | |
| DART | 21,577,652,305 | 21,721,743,786 | 22,922,343,786 |
| UDART | | | 125,115,565,696 |
| Chuo cha Serikali za Mitaa | 10,535,182,220 | 10,745,182,213 | 11,922,250,620 |
| Bodi ya Mikopo ya Serikali za Mitaa | 4,131,215,065 | 3,506,815,065 | 4,220,037,839 |
| TARURA | 5,600,000,000 | 7,000,000,000 | 5,400,000,000 |
| KMC | 11,948,802,000 | 11,489,598,000 | 11,489,598,000 |
| Makao Makuu ya Mikoa | 315,939,400 | 306,079,400 | 305,050,361, |
| Halmashauri | 1,356,340,664,000 | 1,680,506,764,000 | 1,966,193,000,000 |
| **JUMLA** | **1,601,044,595,990** | **1,924,236,488,464** | **2,336,528,152,302** |


**Chanzo:** *Randama ya Wizara pamoja na Usanifu wa Kamati (Aprili, 1, 2026)*


Mwenendo wa Upangaji wa maduhuli kwa

Kielelezo Na 11. *Ulinganisho wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa miaka mitatu mfululizo (2024/2025 hadi 2026/2027 – OWM TAMISEM*




Chanzo: Randama ya Wizara pamoja na Usanifuw a Kamati (Aprili, 1, 2026)

## 4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 – OWM-TAMISEMI

### a) Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya OWM-TAMISEMI kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027

**Mheshimiwa Spika,** katika Mwaka wa Fedha 2026/2027 OWM-TAMISEMI (Fungu 56), Tume ya Utumishi wa Walimu (Fungu 02), na Sekretarieti za Mikoa (Mafungu 26) inaomba kuidhinishiwa kiasi cha shilingi **12,268,472,643,000.** Kati ya hizo shilingi **8,542,154,664,000, sawa na asilimia 69** ni kwa ajili ya matumizi ya

kawaida na shilingi **3,726,317,979,000** sawa na asilimia 31 ni kwa ajili ya matumizi ya maendeleo (Tazama kielelezo Namba 12) . Kati ya fedha za matumizi ya kawaida zilizoombwa shilingi **6,844,897,496,000** sawa na asilimia 80.1 zimetengwa kwa ajili ya mishahara na **shilingi 1,697,257,168,000**, sawa na asilimia 19.86 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo. Aidha, kati ya shilingi **3,726,317,979,000** za miradi ya maendeleo shilingi **2,938,501,239,000,** sawa na asilimia 78.8 ni fedha za ndani na shilingi 787,816,740,000 sawa na asilimia 21.2 ni fedha za nje.


**b) Uwiano wa Mpango wa Bajeti ya Matumizi ya Wizara (Fungu 56, Fungu 02 pamoja na Mafungu 26 ya Sekretarieti za Mikoa) kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027 na bajeti ya Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026;**


**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanya uchambuzi wa kina na kulinganisha mpango wa bajeti wa mwaka 2026/2027 na bajeti ya Wizara hiyo kwa mwaka 2025/2026. Nia ni kupima mabadiliko ya matumizi na mapato katika Wizara na kufuatilia utekelezaji wa mipango kama ilivyokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,** katika uchambuzi wa bajeti, Kamati imebaini kuwa kuna ongezeko la upangaji wa bajeti ya Wizara kutoka **Shilingi 11,612,594,336,000** kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026 hadi **Shilingi 12,268,472,643,000** kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, sawa na ongezeko la **Shilingi 655,878,307,000** ambalo ni sawa na **asilimia 5.6.** Aidha, matumizi ya kawaida yameongezeka kutoka **Shilingi 7,836,140,708,000** hadi **Shilingi 8,542,154,664,000** sawa na ongezeko la **Shilingi 706,013,956,000,** sawa na **asilimia 9** huku

matumizi ya maendeleo yakipungua kutoka **Shilingi 3,776,453,628,000** hadi **Shilingi 3,726,317,979,000** ikiwa ni punguzo la **Shilingi 50,135,649,000** sawa na **asilimia 1.33**.

Kielelezo Na. 12: Sura ya utengaji wa Makisio ya matumizi ya kawaida na maendeleo (OWM – TAMISEMI kwa mwaka 2026/2027








**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilibaini kuwa matumizi ya kawaida kwa upande wa mishahara yameongezeka kutoka **Shilingi 6,292,557,648,000** kwa Mwaka 2025/2026 hadi **Shilingi 6,844,897,496,000** katika Mwaka 2026/2027; sawa na ongezeko la **Shilingi 552,339,848,000**, sawa na **asilimia 8.78** na kwa upande wa matumizi mengineyo yameongezeka kutoka **Shilingi 1,543,583,060,000** hadi **Shilingi 1,697,257,168,000** sawa na ongezeko

la **Shilingi 153,674,108,000** sawa na **asilimia 9.96.** Aidha, matumizi ya maendeleo kwa upande wa fedha za ndani yameongezeka kutoka **Shilingi 2,496,431,476,000** mwaka 2025/2026 hadi **Shilingi 2,938,501,239,000** kwa Mwaka 2026/2027 sawa na ongezeko la **Shilingi 442,069,763,000** sawa na **asilimia 17.7;** huku matumizi ya maendeleo kwa upande wa fedha za nje yamepungua kutoka **Shilingi 1,280,022,152,000** kwa Mwaka 2025/2026 hadi **Shilingi 787,816,740,000** kwa Mwaka 2026/2027 sawa na punguzo la **Shilingi 492,205,412,000** sawa na **asilmia 38.45**; kama inavyoonekana katika kielelezo Namba 13 na Jedwali Namba 6.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilihoji sababu ya kupungua fedha za nje kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo. Wizara imeeleza kuwa, miongoni mwa sababu zilizopelekea kupungua kwa bajeti hiyo ni kubadilika kwa sera za washirika wa maendeleo ambazo zimeathiri mapokezi ya fedha za maendeleo za nje.

Kielelezo Na. 13: Mwenendo wa upangaji wa Bajeti OWM-TAMISEMI kuanzia mwaka 2024/2025 hadi 2026/2027



**JEDWALI NA 6:** ***Ulinganisho wa Bejeti (Fungu 56, Fungu 02 na Mafungu 26 ya Mikoa) kwa Mwaka wa Fedha 2024/2025 Hadi 2026/2027***

| MATUMIZI | 2024/2025 | 2025/2026 | 2026/2027 |
|---|---|---|---|
| Mishahara | 5,524,636,066,000 | 6,292,557,648,000 | 6,844,897,496,000 |
| OC | 1,185,339,122,500 | 1,543,583,060,000 | 1,697,257,168,000 |
| Maendeleo Ndani | 2,269,830,464,000 | 2,496,431,476,000 | 2,938,501,239,000 |
| Maendeleo Nje | 1,145,414,750,667 | 1,280,022,152,000 | 787,816,740,000 |
| **Jumla** | **10,125,220,403,167** | **11,612,594,336,000** | **12,268,472,643,000** |

***Chanzo**: Randama ya Wizara na usanifu wa Kamati*

**Mheshimiwa Spika**, Kamati inapongeza jitihada inayoendelea kufanywa na Wizara katika upangaji wa bajeti ya maendeleo kwa kutumia mapato ya ndani. Hii itapelekea kuondokana na utegemezi wa fedha za wafadhili, kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya ndani kwa kuongeza juhudi katika ukusanyaji wa mapato na kuendelea kuibua vyanzo vipya vya mapato pamoja na kuboresha uwajibikaji na usimamizi wa fedha.

## SEHEMU YA TANO

## 5.0 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika,** Baada ya Uchambuzi wa bajeti, Kamati inatoa Maoni, Ushauri na Mapendekezo yafuatayo kwa lengo la Kuboresha Utendaji kazi wa Wizara hii katika kuwahudumia wananchi: -

### (a) Upungufu wa matundu ya vyoo katika Shule za Msingi na Sekondari

**Mheshimiwa Spika,** katika taarifa ya Kamati iliyotolewa Katika Bunge lako Tukufu kuhusu Utekelezaji wa Bajeti ya iliyokuwa OR-TAMISEMI, kamatili iliwasilisha maoni yake. Moja ya maoni ilikuwa ni kuhusu kufanya tathmini ya upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini, pamoja na kuelezea mikakati ya utatuzi wa changamoto hiyo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inaipongeza Serikali kwa kufanya jitihada za kutatua changamoto hiyo. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa changamoto hiyo bado ni kubwa ukilinganisha na juhudi zilizochukuliwa na Serikali katika kutenga bajeti na kujenga matundu ya vyoo. Wakati wa uchambuzi wa taarifa za bajeti za halmashauri mbalimbali zilizowasilishwa mbele ya Kamati, Kamati ilibaini kuwa pamoja na jitihada zilizowekwa na Serikali katika kufanya tathmini ya uhitaji wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini na katika ujenzi wa matundu ya vyoo, bado kuna upungufu wa matundu vya vyoo katika shule nyingi nchini.

**Mheshimiwa Spika,** kutokana na hali hiyo kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

(i) Wizara ifanye tathmini upya kuhusu mahitaji halisi ya upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini ;

(ii) Pamoja na Halmashauri nchini kuchukua hatua mbalimbali katika kutatua changamoto hii, Kamati inashauri Wizara pia kuweka mkakati wa kuzisaidia Halmashauri kutatua tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini;

(iii) Halmashauri pamoja na Wizara ya OWM-TAMISEMI kuwashirikisha wadau mbalimbali kushiriki katika kutatua tatizo la upungufu wa matundu ya vyoo katika shule za msingi na sekondari nchini.

(b) **Ujenzi wa Shule za Michepuo ya Kiingereza Nchini**

**Mheshimiwa Spika,** vilevile katika taarifa ya Kamati iliyowailishwa katika Bunge lako Tukufu wakati wa Mkutano wa Bajeti Aprili 16, 2025 Kamati ilitoa maoni na ushauri kuhusu utekelezaji wa ujenzi wa shule za mchepuo wa lugha ya kiingereza.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilieleza kwa kina athari zinazoweza kujitokeza ikiwa Serikali itaendelea kujenga shule zenye mlengo wa ufundishaji kwa lugha ya kiingereza. Kamati ilishauri kwa ufasaha kwamba Halmashauri nchini ziache kabisa kuteleza miradi hiyo isipokuwa kwa kibali maalum cha OWM-TAMISEMI na kwa sababu za msingi za uanzishwaji wa shule hizo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inapongeza Halmashauri zilizotekeleza ushauri huo kwa umakini na kwa ufanisi. Hata hivyo kuna baadhi ya halmashauri zimeendelea kutekelza miradi hiyo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inaendelea kusisitiza halmahsuri nchini kufuata ushauri kama ulivyotolewa na Bunge katika Mkutano wa 19 wa Bunge la 12.

**(c) Mwongozo wa utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu**

**Mheshimiwa Spika,** Serikali imeanza kutoa mikopo ya asilimia 10 kwa ajili ya wanawake, vijana na wenye ulemavu baada ya miongozo mbalimbali kuwekwa sawa. Hata hivyo, Kamati imebaini kuwa katika utoaji wa mikopo ya asilimia 10 kwa wanawake, vijana na watu wenye ulemavu, baadhi ya halmashauri hazikufuata kanuni ya utoaji wa mikopo ya 4:4:2; huku Halmashauri nyingine zikishindwa kusimamia utaratibu uliowekwa kuhusu urejeshaji wa mikopo hiyo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

(i) Halmashauri zizingatie utoaji wa mikopo kwa uwiano wa 4:4:2 kama inavyotakiwa bila ubaguzi wowote wa jinsi, au hali ya ulemavu;

(ii) Halmashauri zizingatie utaratibu wa kisheria uliowekwa kuhusu fedha za marejesho zinazorejeshwa na wanufaika wa mikopo hiyo;

(iii) Katika halmashauri nyingi nchini watu wenye ulemavu hawakufikiwa na mikopo hii kwa madai ya kukosekana

kwa vikundi vya watu wenye ulemavu au vikundi hivyo kukosa vigezo na hivyo kukosa kunufaika kama ilivyokusudiwa;

(iv) Halmashauri ziweke mikakati ya kutoa elimu kwa wananchi kuhusu namna na vigezo vya utaji wa mikopo hiyo;

(v) Ikiwa Halmashauri zina ukwasi wa fedha zinazotokana na marejesho au utengaji wa fedha hizo, Halmashauri hiyo iombe kibali kutoka OWM-TAMISEMI kufanya ugawaji upya (reallocation) wa fedha hizo kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa utaratibu utakaokubaliwa na OWM-TAMISEMI.

**(d) Uzalishaji wa Madeni ya Watumishi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilitoa maoni na ushauri kwa OWM-TAMISEMI kuhusu kuweka mkakati wa kumaliza madeni ya watumishi katika Halmashauri nchini. Kamati imetaarifiwa kuwa utekelezaji huo unaendelea. Hata hivyo, wakati wa uchambuzi wa utekelezaji wa bajeti ya Mwaka 2025/2026 Kamati ilibaini kuwa zipo halmashauri ambazo zimeendelea kuzalisha madeni mapya ya watumishi, kinyume na maoni na ushauri wa Kamati. Kutoka na hali hiyo, kamati inaendelea kutoa maoni na ushauri kama ifuatavyo: -

(i) Halmashauri ziache kuzalisha madeni mapya yasiyo ya lazima ya watumishi;

(ii) Ofisi ya Waziri Mkuu – TAMISEMI pamoja na Halmashauri zitenge bajeti ya kuhakikisha kuwa madeni yaliyopo ya watumishi yanalipwa;

(iii) OWM-TAMISEMI iweke mkakati wa kusaidia jitihada zinazofanywa na Halmashauri nchini za kulipa madeni ya watumishi.

**(e) Upungufu wa Watumishi**

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini kwamba katika halmashauri nyingi nchini kuna upungufu wa watumishi hususan katika sekta za afya, elimu na uhandisi**.** Hii imepelekea baadhi ya shughuli kama vile utekelezaji wa miradi ya maendeleo na utoaji wa huduma katika halmashauri zenye upungufu wa watumishi kutofanyika kwa ufanisi na hivyo kushuka kwa ubora wa huduma hizo. Kutokana na hali hiyo, Kamati inatoa ushauri kama ifuatavyo: -

(i) OWM-TAMISEMI pamoja na Halmashauri nchini zifanye msawazo wa watumishi ili kupunguza ukali wa tatizo la upungufu wa watumishi katika maeneo yenye upungufu mkubwa;

(ii) Serikali kuendelea kutenga bajeti kwa ajili ya kuajiri watumishi katika kada zenye upungufu mkubwa wa watumishi katika Halmashauri nchini;

**(f) Miradi Kutokukamilika kwa Wakati**

**Mheshimiwa Spika,** kuna baadhi ya miradi ya maendeleo katika halmashauri mbalimbali nchini haijakamilika ndani ya muda uliopangwa na hivyo kushindwa kuleta tija iliyokusudiwa katika jamii. Aidha, kuchelewa au kutokupelekwa kwa fedha za miradi ya maendeleo hususan katika miradi ambayo ilikuwa ikitegemea fedha za nje katika utekelezaji wake ni miongoni mwa sababu zilizopelekea miradi hiyo kutokukamilika kwa wakati. Kutokana na hali hiyo Kamati inatoa ushauri ufuatao: -

(i) OWM-TAMISEMI iimarishe vitengo vya ufuatiliaji na tathmini (monitoring and evaluation) ili vitengo hivyo vitekeleze jukumu la kuimarisha ufuatiliaji na tathmini kwenye miradi yote katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa ufanisi;

(ii) Serikali iendelee kubuni vyanzo vipya pamoja na kuimarisha vyanzo vyote vya mapato ili kuzifanya Halmashauri nchini, pamoja na Taifa kwa ujumla kutegemea kwa asilimia kubwa fedha za ndani katika utekelezaji wa miradi yake.

**SEHEMU YA SITA**

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, kwa mara nyingine ninapenda kutoa shukrani zangu kwako kwa fursa uliyonipa ya kuwasilisha maoni haya ya Kamati lakini pia kwa kuendelea kuliongoza vyema Bunge letu Tukufu. Ninawashukuru sana Mheshimiwa Prof. **Riziki Silas Shemdoe** (Mb) – Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Reuben **Nhamanilo Kwagwilwa (Mb)** Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa na Mheshimiwa **Jafar Rajab Seif (Mb)** Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano wanaoipa Kamati. Aidha, ninamshukuru Katibu Mkuu Wizara ya TAMISEMI, Ndg. Adolf Ndunguru, Naibu Makatibu Wakuu, Prof. Mary Nagu, Ndg. Sospeter Mtwale, Ndg. Eng. Rogatus Mativila na Ndg. Atupele Mwambene, pamoja na Watendaji wote wa Wizara na Taasisi zake kwa ushirikiano ambao wamekuwa wakiipa Kamati tangu tulipoanza kufanya nao kazi na kushiriki vizuri kwenye uchambuzi wa Bajeti ya Wizara hii.

**Mheshimiwa Spika,** kipekee ninawashukuru sana Wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Mheshimiwa Jafari Wambura Chege (Mb), Makamu Mwenyekiti wa Kamati kwa ushirikiano mzuri ambao wananipa. Wajumbe hawa ni wachapa kazi na wameshiriki kikamilifu katika uchambuzi wa Bajeti na kuhakikisha wanahoji ili kupata ufafanuzi wa kina. Ninawapongeza sana na ninaomba kuwatambua kwa majina kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Florent Laurent Kyombo – **Mwenyekiti**

2. Mhe. Jafari Wambura Chege – **M/Mwenyekiti**
3. Mhe. Zacharia Paulo Isaay – Mjumbe
4. Mhe. Margaret Semwanza Sitta – Mjumbe
5. Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis “
6. Mhe. Hawa Subira Mwaifunga “
7. Mhe. John Fransisco Nzilanyingi “
8. Mhe. John John Nchimbi “
9. Mhe. Asha Omr Rashid “
10. Mhe. Lucy Edward Mwakyembe “
11. Mhe. Jesca John Magufuli “
12. Mhe. Tamima Haji Abass “
13. Mhe. Alaudin Hasham Salim “
14. Mhe. Benjamin Lukubha Ngayiwa “
15. Mhe. Abdallah Jafari Chaurembo “
16. Mhe. Moses Ludovico Kaegele “
17. Mhe. Lucy Thomas Mayenga “
18. Mhe. Wilson Charles Mahera “
19. Mhe. Mariam Abdallah Ibrahim “
20. Mhe. Kassim Ali Khamis “
21. Mhe. Henry Charles Kabeho “
22. Mhe. Agnesta Lambert Kaiza “
23. Mhe. Silvestry Francis Koka, Mb “
24. Mhe. Mary Daniel Surati “

**Mheshimiwa Spika**, ninapenda kuwashukuru Watumishi wote wa Ofisi ya Bunge chini ya Uongozi wa Katibu wetu wa Bunge Ndg. Baraka I Leonard, kwa kuiwezesha Kamati kutekeleza majukumu

yake vyema. Pamoja naye ninamshukuru Mkurugenzi wa Idara ya kamati za Bunge Ndg. Athumani Brambat, *ndc*, Wakurugenzi Wasaidizi Ndg. Michael Chikokoto, *ndc,* na Ndg. Gerald Magili kwa ushirikiano wanaoipa Kamati yetu wakati wote.

**Mheshimiwa Spika,** baada ya maelezo hayo, sasa ninaliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi zilizo chini yake kwa Mwaka wa Fedha 2026/2027, kama yalivyowasilishwa na mtoa hoja, **Fungu 56, 02, 36 ,47, 54, 63, 70, 71, 72, 79, 74, 75, 76, 77, 78, 79, 80, 81, 82, 83, 84, 85, 86, 87, 88, 89, 90, na 95**

**Mheshimiwa Spika,** ninaomba kuwasilisha, naunga mkono Hoja.

Florent Laurent Kyombo (Mb),

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

01 APRILI, 2026